Alhamisi Februari 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580859
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US









**Mwanafunzi** adaiwa kuuawa kwa kukatwa mapanga na kaka yake

UKURASA 3

**MBAPPE AFUNGUKA KUHUSU UBORA WAKE**

UKURASA 21

# Utendaji TANESCO walishtua Bunge



Mkurugenzi Mtendaji TANESCO, Maharage Chande

• **Wadai** shirika na STAMICO wanafanya kazi nchi mbili tofauti... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Makamba

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MWILI WA DK. MWELE SASA KUWASILI KESHO**

MWILI wa Mkurugenzi wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele katika Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Mwele Malecela...

## Nape atoa msimamo madai wizi wa 'bando'

UKURASA 3




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi zawadi maalum ya mlango wa Zanzibar (Zanzibar Door) Makamu wa Rais Mtendaji wa Benki ya AFREXIM, Amr Kamel, baada ya mazungumzo yao yaliofanyika Ikulu, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Wabunge waitaka ripoti ya uchunguzi moto soko Kariakoo



UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA SC: USHINDI JADI YETU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na ujumbe wa Benki ya Afrexim kutoka nchini Misri ukiongozwa na Makamu wa Rais Mtendaji, Amr Kamel (kulia kwa Rais), Ikulu Zanzibar jana. Watano kulia ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaban na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi, Zena Ahmed Said. **PICHA: IKULU**

# Utendaji TANESCO walishtua Bunge

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imesema imebaini kuwa taasisi nyingi za umma zinafanya kazi kama nchi mbili zenye mirengo tofauti.

Baadhi ya taasisi hizo ni Shirika la Umeme (TANESCO) ambalo kamati hiyo imesema limeshindwa kuunganisha umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo unaosimamiwa na kampuni ya STAMIGOLD inayomilikiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Hali hiyo imebainika na kamati baada ya kuona taasisi nyingi za umma hazifanyi kazi kwa kushirikiana licha ya dhamira za taasisi zote kuwa kujenga uchumi imara wa Tanzania.

Akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo bungeni jijini Dodoma jana, Mwenyekiti wake, Jerry Silaa, alisema Bunge linaitaka serikali kuhakikisha kila taasisi inatekeleza wajibu wake kwa wakati na kwa ufanisi ili kurahisisha utekelezaji wa miradi na majukumu ya taasisi zingine.

Jerry alisema Bunge linaitaka serikali ihakikishe TANESCO inaharakisha upelekaji wa umeme katika mgodi huo pamoja na miradi mingine ya kimakakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na taasisi hizo.

"Kumekuwa na changamoto ya baadhi ya taasisi za umma kushindwa kusikilizana na kufanya kazi pamoja kwa maslahi mapana ya nchi.

"Kukosekana kwa ushirikiano katika utekelezaji wa baadhi ya miradi kunakwamisha utendaji wa taasisi nyingine na kuongeza gharama za uendeshaji kama ilivyotokea kwa TANESCO kushindwa kupeleka umeme," alifafanua.

Aliongeza: "Kamati ilipokea taarifa ya uchambuzi wa Msajili wa Hazina pamoja na maelezo ya uongozi wa STAMICO kuhusu tija ya mitaji ya umma iliyowekezwa katika shirika hilo. "Wakati wa majadiliano, kamati ilibaini changamoto kubwa ya kukosekana kwa umeme katika mgodi wa Biharamulo. Mgodi huu unasimamiwa na kampuni ya STAMIGOLD ambayo inamilikiwa na STAMICO kwa asilimia 99."

Alisema kamati ilibaini shughuli za uzalishaji katika mgodi huo ambazo ni uendeshaji mitambo na vifaa vya uchimbaji (mining equipment) pamoja na uchenjuaji (processing) zinategemea kwa kiasi kikubwa nishati ya umeme, lakini kutokana na kukosekana kwa umeme, shirika linalazimika kutumia nishati ya mafuta ya dizeli kuendesha shughuli za uzalishaji (uchimbaji na uchenjuaji).

Kwa mujibu wa kiongozi huyo wa kamati, shirika linatumia kiasi cha mafuta kisichopungua lita 600,000 kila mwezi, huku mahitaji kwa ajili ya ufuaji umeme pekee ni takribani lita 360,000, ikiwa ni wastani wa Sh. 2,500 kwa lita, hivyo mgodi huhitaji Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizeli kila mwezi.

"Mahitaji ya umeme ya shirika kwa mwezi ni wastani wa Uniti 1,368,194, sawa na Sh. 337,571,836.94 (milioni 337.572) pindi TANESCO itakapokamilisha kuunganisha mgodi kwenye gridi ya taifa, Kampuni ya STAMIGOLD itaokoa Sh. milioni 662 kwa mwezi (kwa makisio ya chini) ambayo ni sawa na Sh. bilioni nane kwa mwaka," alisema.

Mwenyekiti huyo ambaye ni Mbunge wa Ukonga, alisema kupungua kwa gharama za uendeshaji wa STAMIGOLD kutaongeza faida itakayoongeza faida kwa kampuni mama STAMICO na hivyo kuongeza gawio kwa serikali.

# Corona yageuzwa maficho biashara dawa za kulevya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema kuwa katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19, baadhi ya Watanzania walitumia mwanya huo kujifanya wagonjwa na kwenda kutibiwa India ilhali wakiwa wamebeba dawa za kulevya.

Hata hivyo, licha ya kutumia mbinu ya kupata vibali vya kutibiwa nje ya nchi kufanya biashara hiyo haramu, walikamatwa kutokana na intelijensia ya wakaguzi kutoka nchi mbalimbali zinazodhibiti dawa hizo.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati wa utoaji mafunzo kwa watumishi wa idara mbalimbali za serikali kuhusu uhamasishaji wa mradi wa upunguzaji madhara kwa watumiaji wa dawa za kulevya mkoani Arusha, Kamishna Jenerali Gerald Kusaya alisema wasafirishaji wa dawa za kulevya wana mbinu mbalimbali za kusafirisha dawa hizo, lakini mamlaka hiyo imewadhibiti.

Alisema katika wimbi la ugonjwa wa UVIKO-19 mwaka jana, wasafirishaji walilitumia kusafirisha dawa hizo kwa kujifanya wanaumwa na wanakwenda kutibiwa India ilhali wakijua kuwa wana dawa za kulevya wanazipeleka huko.

Aliwaomba watumishi wa afya kuwa makini wanapotoa vibali vya wagonjwa kusafiri kwa kuwa inapotokea msafirishaji wa dawa hizo anakamatwa na dawa za kulevya huku amepata kibali cha matibabu kwenda nje ya nchi inashangaza na kuwa fedheha kwa kada ya afya.

"Haiwezekani mtu anaomba kibali kwenda nje ya nchi anapewa halafu katika ugonjwa wa UVIKO-19 anakwenda kutibiwa, ukimwangalia huyo mgonjwa mwenyewe unajiuliza sana!

"Watu wa afya mtusaidie katika hili, maana watumiaji wa dawa za kulevya au wasafirishaji wana mbinu nyingi na hata ukiondoka Tanzania salama, utakamatwa nje ya nchi na dawa zako na kifungo ni maisha au miaka 20 hadi 30 jela," alionya.

Alisema mamlaka hiyo hadi sasa imeshakamata wafanyabiashara wakubwa kadhaa na wengine wanatumikia vifungo gerezani na kusisitiza kuwa mamlaka hiyo ipo macho usiku na mchana, kudhibiti dawa hizo kuingizwa nchini. Alibainisha kuwa mwaka jana dawa za kulevya kilo 859 zilikamatwa na kusisitiza kuwa mamlaka hiyo imejipanga vyema kukamata dawa mbalimbali zinazoingia nchini, ikiwamo bangi na mirungi na ndio maana elimu inatolewa vyuoni na shuleni ili kudhibiti dawa za kulevya zinazoathiri akili.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alitoa rai kwa jamii kuhakikisha inatokomeza dawa hizo zinazoua nguvukazi kwa vijana na kusisitiza kuwa Arusha bado kuna tatizo la kushamiri kwa kilimo cha bangi maeneo ya milimani.

Alisema vyombo vya ulinzi na usalama vinapambana ili kudhibiti kilimo hicho na maeneo ya mipakani ikiwamo kwenye njia za usafirishaji kupitia mabasi.

# Wabunge waitaka ripoti uchunguzi moto Kariakoo

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE wametaka ripoti juu ya kuungua kwa Soko Kuu la Kariakoo jijini Dar es Salaam huku wakiiomba serikali kufanya uchunguzi wa kuungua kwa masoko mara kwa mara.

Rai hiyo ya wabunge ilitolewa juzi wakati wakichangia taarifa ya Kamati za Kudumu za Bunge za Katiba na Sheria, na ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rehema Migila, alisema kila siku kuna taarifa za kuungua kwa masoko, lakini chanzo chake hakielezwi.

"Masoko yamegharimu fedha nyingi sana lakini hayana ufanisi. Mfano Soko la Ndugai limegharimu fedha nyingi lakini uzalishaji wake haueleweki, yametumia fedha nyingi lakini yanaungua kila siku.

"Naiomba serikali pamoja na kwamba inajenga masoko, tunaambiwa tuweke vifaa vya kuzimia moto, vinasaidia nini ikiwa kila siku yanaungua moto? Nashauri kila soko kuwa na mashine za viashiria vya moto ili kusaidia," alisema. Pia alisema ni muhimu wafanyabiashara kwenye masoko wakalazimishwa kuwa na bima ya biashara itakayowasaidia kwenye majanga mbalimbali kama ya moto. "Tunaona wafanyabiashra wanapata hasara lakini benki zinaambiwa ziwaongezee muda wa kulipa, ili nini? wakati mitaji yao imeteketea, bima itakuwa ni suluhisho kulinda mitaji yao," alisema Migila.

Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo, alisema Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) walitembelea soko hilo na kuunda timu ya uchunguzi lakini hadi sasa hakuna taarifa.

Pia alisema suala la kuungua masoko lisichukuliwe kwa urahisi bali liangaliwe kwa jicho la tatu kwa kuwa linarudisha nyuma maendeleo. Katika kipindi cha miezi saba iliyopita, kuna matukio matano ya masoko kuungua nchini. Julai 10, 2021, Soko Kuu la Karikoo liliteketea kwa moto na chanzo chake hakijawekwa bayana hadi sasa.

Usiku wa kuamkia Januari 16, mwaka huu, Soko la Karume liliungua na kusababisha hasara ya Sh. bilioni 7.2. Ripoti ya uchunguzi wa moto huo ilibainisha kuwa chanzo chake ni mshumaa uliowashwa na 'mateja' waliokuwapo sokoni huko waliokuwa wanavuta bangi katika moja ya vibanda.

Februari Mosi mwaka huu, Soko la Mbuyuni, Moshi mkoani Kilimanjaro liliripotiwa kuungua. Pia vibanda vitatu katika soko hilo viliripotiwa kuteketea kwa moto juzi.

Usiku wa kuamkia Februari 13 mwaka huu, Soko la Mbagala Rangitatu liliungua huku kukiundwa kamati ya kuchunguza chanzo chake.

# Mil. 300/- leseni za biashara zayeyuka

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

ZAIDI ya Sh. milioni 300 zitokanazo na malipo ya leseni za biashara wilayani Bukoba mkoani Kagera, zimebainiwa kutoonekana katika mfumo baada ya kufanya uchunguzi kwenye idara ya biashara ya Manispaa ya Bukoba.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali, alibainisha hayo jana wakati akizungumzia taratibu na mabadiliko ya ukataji wa leseni kwa wafanyabiashara wa Manispaa ya Bukoba.

Machali alisema hali hiyo imelazimu kuunda kamati ya kwenda kufanya msako wa leseni ambazo zimelipiwa na kutoonekana katika mfumo kupitia maduka na maeneo ya biashara.

"Lakini ninapoongea hapa, tayari kuna kamati itaanza kesho itakayopita duka kwa duka kujiridhisha na leseni zilizoko na zilizofanya kuonekana kuna malipo lakini pesa hazipo," alisema Machali.

Alisema wafanyabiashara wanafika kulipia ada ya leseni na kuacha pesa lakini haifiki serikalini badala yake kuingizwa mfukoni.

"Mfano mimi ndiye nakata leseni unakuta natengeneza namba A malipo yenye Sh. 100,000 hiyo ni upande wa serikali lakini mteja ametoa Sh. 300,000, Sh. 200,000 zote nakunja naweka mfukoni," alisema Machali.

Alisema mfanyabiashara akija kuchukua leseni kwa sababu kile ni kitabu atachaniwa na kupewa karatasi ya Sh. 300,000 na hajui aliyolipa halali ni Sh. 100,000.

Machali alisema vitendo hivyo vinafanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu kazini na kusababisha serikali kukosa mapato ya kuendesha miradi yake.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, Hamid Njovu, alisema usajili wa mfumo hufanya kutambua aina ya biashara inayofanywa na mhusika na kufuatilia malipo anayostahili kulipa.

Njovu alisema endapo mfanyabishara amemaliza malipo yake, anatakiwa apewe stakabadhi inayoonyesha malipo na kiasi cha pesa aliyotoa kabla hajapokea leseni aliyokata.

Hata hivyo, alisema leseni ina hatua tano ambazo ni uombaji wa kuwa na biashara na kuitambua, utambulisho wa namba ya mlipakodi, hati ya msawazo na usajili katika mfumo.

# Nape atoa msimamo madai wizi wa 'bando'

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

SERIKALI imetoa maelezo kuhusiana na kuwapo kwa malalamiko ya wizi wa 'bandle' la simu.

Maelezo hayo yametolewa na Waziri wa habari, Mawasiliano na Teknolojia ya habari, Nape Nnauye bungeni.

Nape alisema kwamba kutokana na malalamiko ya watumiaji wa 'bandle la simu, serikali ilifanya tathmini, ambayo imebainisha kwamba hayana ukweli, bali zinakwisha kutokana na simu za kisasa wanazotumia watu.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge na kamati ambao wamelalamika kwa wizi wa bandle, Nape , alisema uwezo wa Mamlaka ya Mawasilinao Tanzania (TCRA), kufuatilia miamlaka mbalimbali umeongezeka.

"Tunaendelea kuchambua taarifa mbalimbali juu ya mamalamiko ya matumizi ya bandle kwenye simu zetu, hoja kwamba kuna zinazowekwa zinatumika bila mtumiaji kuzitumia, yamekuwapo malalamiko yamefikishwa kwenye mamlaka husika na uchambuzi umefanyika," alisema na kuongeza:

"Matokeo ya uchambuzi yanaonyesha hakuna wizi uliotokea isipokuwa kuna tatizo la matumizi ya simu za kisasa, yamejikita kwenye simu za kisasa baadhi ya 'application' zinatumia 'bandle' bila mwenye simu kujua, nyingine simu hizo unaweza kuweka bandle na kuwasha 'data' kupitia 'hot sport; ambayo inatumiwa na mtu mwingine."

"Kuna watu wamechunguzwa ikabainika kuna watu wametumia bandle zao."

Alisema suluhisho lililoletwa ni kupitia Baraza la Watumiaji wa Huduma za Simu ambao wametengeneza 'application' ya mtumiaji wa simu kufuatilia matumizi yake na ataweza kuzima baadhi ya 'application' zinazotumia mtandao wake.

"Tunafanya majaribio ya 'application hiyo na itakapokuwa tayari watumiaji watapewa na kufuatilia. Pia tunatoa elimu ya matumizi ya simu za kisasa ili watu wasiingie kwenye gharama kwa kutokujua," alisema Nape.

Aidha, alisema utafiti umeonyesha shida kubwa ni kwenye matumizi badala ya wizi na kwamba hadi sasa hawajakamata wizi wowote.

"Jambo hili limekuwa kubwa na linazungumzwa muda mrefu, ni rahisi kudhani kuna wizi na tukawahukumu watoa huduma lakini TCRA, malalamiko yoyote hakuna lalamiko limethibitisho kuna wizi, bado yanaendelea kupokelewa,"alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, alisema wanaishauri serikali iisimamie TCRA kukutana na wadau na watoa huduma, ili kuona chanzo cha kupungua kwa miamala ya simu kwa lengo la kutatua changamoto hizo.

"Kamati ilibaini kupungua kwa miamala ya simu, jambo linalokinzana na matarajio ya kisera katika sekta. Kupungua kwa miamala hiyo ya simu ni ishara ya changamoto ya shughuli za umma za udhibiti na uendeshaji wa sekta ya mawasiliano, hali inayohitaji kurekebishwa mapema,"alisema.



Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, akihutubia washiriki wa kozi ya ulinzi na mafunzo ya kimkakati katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanafunzi adaiwa kuuawa kwa mapanga na kaka yake

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

MWANAFUNZI wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Mwenge, Manispaa ya Morogoro, Faidhat Ibrahim (13) anadaiwa kuuawa kwa kukatwa na mapanga na kaka yake, Shomari Malima.

Faidhat anadaiwa kufanyiwa kitendo hicho kilichompotezea uhai wake nyumbani kwao, mtaa wa Tambukareli, kata ya Kingolwila, huku sababu ikitajwa ni ugomvi wa kifamilia kati ya mama wa marehemu na wa mtuhumiwa.

Akisimulia mkasa huo, mama wa marehemu, Zawadi Kidukulu, alisema tukio hilo lilitokea juzi huku akilihusisha na ugomvi wa kifamilia kwa sababu awali aligombana na dada yake baada ya yeye na mume wake kulima mihogo katika shamba la dada yake kwa kuwa alikabidhiwa kulinda eneo wakati hayupo.

Zawadi alisema wakati mazao hayo yamekuwa tayari kuvunwa, dada yake ambaye alikuwa akiishi Ngerengere, alirudi na kuvuna mazao hayo bila kumjulisha na alipohoji ndipo ugomvi ukazuka kitendo ambacho anaamini kiliingiza chuki hata kwa mtoto wake hadi kufikia hatua ya kutekeleza mauaji hayo.

"Ni kweli tulikuwa na ugomvi mimi na dada yangu. Itakuwa ndiye kapandikiza chuki hadi kwa mtoto wake kwa sababu hata mwanagu alikuwa akikutana naye akimsalimia haitikii. Lakini sikujua kama itafikia hatua ya kumtoa roho mwanangu kwa sababu ugomvi haukuwa mkubwa kiasi hicho," alisema Zawadi.

Ibrahim Gaddafi, baba wa marehemu, alisema mara ya mwisho kuzungumza na mtoto wake ilikuwa juzi baada ya kutoka shuleni ambapo alimuomba dada yake aende kumfuata mama yake ambaye alikuwa kazini.

Alisema baada ya kumfuata mke wake ambaye anafanya kazi ya kupasua kokoto, alipigiwa simu kuwa mtuhumiwa ameleta vurugu kwa mama yake lakini kabla hawajafika akapigiwa simu kuwa mtuhumiwa amempiga mtoto wake na yuko katika hali mbaya.

"Wakati tuko njiani tunaenda kwa shemeji yangu, ndipo nikapigiwa tena simu na kuambiwa nirudi nyumbani kwangu Faidhat amepigwa na kaka yake, yaani baada ya kutoka kwenye ugomvi na mama yake ndipo akaja huku kwangu," alisema Gaddafi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tambukareli, Juma Muitano, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12:30 jioni. Alisema baada ya kupata taarifa, wakazi wa mtaa huo walianza msako wa kumtafuta mtuhumiwa bila mafanikio.

Aliwataka wakazi wa mtaa huo kuwa na utamaduni wa kuripoti taarifa za migogoro hasa ya kifamilia pindi inapotokea ili kupatiwa ufumbuzi kisheria na kuondokana na madhara makubwa yanayoweza kutokea.

Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP), Ralph Meela, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba Jeshi la Polisi linamshikilia mama wa mtuhumiwa baada ya uchunguzi wa awali kuonyesha ni mgogoro wa kifamilia baada ya mtuhumiwa kukimbia.

Alisema jeshi hilo linaendelea kumtafuta mtuhumiwa ili kubaini sababu hasa za mauaji hayo na kwamba pamoja na mambo mengine pia mtuhumiwa huyo anadaiwa aliwahi kuhusika na mauaji katika kijiji cha Ngerengere miaka ya nyuma.

"Ziko sababu nyingi zinazohusishwa na mauji haya, kubwa likiwa mgogoro wa kifamilia pamoja na ushirikina kwamba mtuhumiwa na mama yake wamekuwa wakimtuhumu mama wa marehemu kuwaroga," alisema.




Fundi akisambaza kokoto kwenye stendi ya mabasi ya Makambako mkoani Njombe jana, baada ya stendi hiyo kuharibika na kusababisha maji kutuama kila mvua zinaponyesha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakili adai ushahidi haukutosha kumtia hatiani, kumfunga Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKILI wa waleta rufani katika kesi ya jinai namba 105 iliyomtia hatiani aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, Mosses Mahuna, amedai kwamba ushahidi uliotolewa mahakamani haukutosheleza kuwatia hatiani washtakiwa kwa makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kutumia genge la uhalifu.

Pia amedai kwamba Jeshi la Polisi lilifanya makosa ya kutokumkamata haraka aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya, kwa madai ya kwamba alikuwa mteule wa Rais, hivyo walitakiwa kupewa kibali cha kumkamata.

Wakili huyo alitoa madai hayo jana wakati wa usikilizwaji wa rufani namba 129 ya Sabaya na wenzake wawili, mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Sedekia Kisanya.

Akiwasilisha hoja ya pili ya kupinga hukumu iliyotolewa mahakamani huko, Wakili Mahuna alidai kwamba utata mwingine katika hukumu hiyo umeonekana pale tukio limetokea na wahusika kuchelewa kukamatwa.

Alidai kwamba kwa mujibu wa shahidi wa saba katika shauri hilo, Inspekta Gwakisa Minga, hawakuwakamata washtakiwa hao hasa mshtakiwa wa kwanza, Sabaya, kwa kuwa alikuwa mteule wa Rais.

"Alikuja hapa mahakamani Inspekta Gwakisa Minga, alitueleza kwamba walichukua muda mrefu kumkamata Sabaya kwa kuwa alikuwa mteule wa Rais. Ilitakiwa wapewe kibali cha kumkamata. Je, swali letu ni kwamba kama mtu alikuwa jambazi wangesubiri kwa kipindi chote kupewa kibali?" Alidai Mahuna.

Wakili Mahuna alidai kwamba hoja ya 13 ya waleta rufani wanalalamika kwamba Mahakama ya Hakimu Mkazi, ilikosea kwa kuwa washtakiwa hao hawakutambuliwa kwa utaratibu na njia sahihi zinazotakiwa.

Kadhalika, alidai kwamba kwa mujibu wa shahidi wa pili wa mashtaka Hajirini Saad, alidai hakukuwa na silaha iliyotumika na Mahakama ya Hakimu Mkazi, ilitoa kosa hilo kutoka kwenye unyang'anyi wa silaha kwenda kwenye unyang'anyi wa kutumia genge.

"Hakuna ushahidi wowote unaothibitisha kuna kiasi cha fedha kiliibwa kwenye shtaka la kwanza kwa kuwa shahidi wa pili aliyetakiwa kuthibitisha hilo alisema hajui kiasi cha fedha kilichoibiwa dukani wala kumwona mtu aliyempiga.

"Shahidi wa sita wa mashtaka, Bakari Msangi, alitueleza hapa mahakamani akiwa kwenye gari wakati wakiondoka dukani, aliona fedha bando mbili za milioni moja moja zikiwa kwenye mfuko wa rangi ya kaki. Pia alidai wakiwa Tulia Lodge, Sabaya alimwonyesha bando moja la fedha huku akimwambia wewe mtoto wa kiswahili umeona hela?" alidai Mahuna.

Katika shtaka la tatu la uporaji wa simu na Sh.35,000 mali ya Ramadhani Ayubu, alidai kuwa shahidi huyo alishindwa kuthibitisha mahakamani kwamba aliibiwa fedha hizo na simu aina ya Tecno Pop 1.

"Mahakama ya Hakimu Mkazi ilipaswa kuwaachia huru katika shtaka hili kwa kuwa shahidi alishindwa kuthibitisha kwamba aliporwa fedha na kunyang'anywa simu yake na ushahidi haukutosha kuwatia hatiani kwa kosa la unyang'anyi kwa kutumia silaha," aliendelea kudai.

Wakili mwingine wa waleta rufani, Majura Magafu, akizungumzia hoja ya tatu, alidai kwamba vielelezo vya ushahidi wa picha na barua iliyopelekwa maabara ya uchunguzi wa kielektroniki vimetengenezwa na vilipokewa mahakamani kinyume cha utaratibu.

Alidai kwamba mkata rufani wa tatu (Daniel Mbira), aliieleza mahakama kuwa siku ya tukio hakuwapo eneo la tukio na hakimu hakuzingatia ushahidi wake wakati akiandaa hukumu hiyo.

"Mahakama ilishindwa kutambua utaratibu wa gwaride la utambuzi ulivyofanyika na tunaona halikuwapo. Pia ilitakiwa kufanya kwa mshtakiwa wa kwanza na mpaka leo hii hakuna ushahidi kwamba washtakiwa wa pili na wa tatu hawakukamatwa na kuhojiwa na kuchukuliwa maelezo ya onyo." Alidai.

# Mwili wa Dk. Mwele kuwasili kesho

**Na Romana Mallya**

MWILI wa Mkurugenzi wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele katika Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Mwele Malecela (58), aliyefariki dunia Alhamisi iliyopita Geneva, Uswisi, unatarajia kuwasili nchini kesho.

Msemaji wa familia, Samuel Malecela, alisema hayo jana wakati akitoa ratiba ya msiba huo na kwamba mwili huo utaagwa jijini Dar es Salaam na Dodoma kabla ya mazoko yatakayofanyika Jumatatu.

Samuel ambaye ni mdogo wa marehemu, alisema mwili huo utasafirishwa kwa ndege Shirika la Ndege la Uholanzi (KLM) na wanatarajia kuupokea katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere kesho usiku.

"Baada ya kuupokea utaletwa hapa nyumbani. Siku ya Jumamosi asubuhi itafanyika sala fupi nyumbani na ndugu kumuaga na baadaye utapelekwa Kanisa Kuu la Anglikana la Mtakatifu Albano, Upanga, Dayosisi ya Dar es Salaam kwa uibada maalum.

"Kuanzia saa 5:00 asubuhi, mwili utapelekwa viwanja vya Karimjee ambako watu watapata nafasi ya kuaga na salamu za rambirambi kutolewa," alisema.

Baada ya tukio hilo, alisema mwili utapelekwa uwanja wa ndege kwa safari ya Dodoma na utapelekwa moja kwa moja Hospitali ya Benjamin Mkapa na Jumapili utapelekwa nyumbani Kilimani ambako na wakazi wa Dodoma watauaga.

Alisema Jumatatu mwili utapelekwa utapelekwa Kanisa Kuu la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT), Dodoma kwa ibada kabla ya kupelekwa Mvumi, wilaya ya Chamwino kwa maziko.

Mwele aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Vituo vya Kudhibiti ndani ya shirika hilo, Kanda ya Afrika na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) hadi Desemba 17, 2016.

Mwaka 2015 katika Uchaguzi Mkuu, alikuwa miongoni mwa wanachama 38 waliochukua fomu kugombea kiti cha urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

# DC aagiza kusitishwa mikataba ujenzi vyoo

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, ameshtukia utendaji mbovu wa makandarasi wanaojenga vyoo katika shule mbalimbali wilayani humo kwa gharama ya Sh. bilioni 3.7 na kuagiza kusitishwa mikataba yao.

Mradi huo unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kupitia ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa.

Makilagi alitoa agizo hilo jana jijini Mwanza, alipokagua ujenzi wa vyoo vya wanafunzi na walimu katika shule mbalimbali wilayani Nyamagana.

Mradi huo unatekelezwa katika shule za msingi za Nyakabungo, Sahara na Azimio zilizoko wilayani humo. Makandarasi katika mradi huo ni kampuni za CF Builders ya Mwanza na GOPA Contractors Tanzania Limited ya mkoani Dar es Salaam.

Kutokana na mwenendo wa ujenzi huo, Makilagi aligiza mikataba ya kampuni hizo kusitishwa ili iwe fundisho kwa makandarasi wengine ambao hawana uzalendo.

"Mkurugenzi (Mtendaji) wa MWAUWASA, (Leonard Msenyele) kaeni na bodi ya wakurugenzi kupitia mikataba hiyo, kushauriana na kisha kusitisha mikataba ya makandarasi hawa ili mtafute makandarasi wazalendo watakaomalizia miradi hiyo na watoto waweze kupata huduma ya choo," alisema.

Makilagi alisema mradi ni mzuri ila makandarasi wameshindwa kufanya kazi vizuri na kwamba serikali hairidhiki na kazi, hivyo inasimamisha mara moja.

"Mimi natoa maelekezo hapa tuanzishe mchakato wa kusitisha mkataba. Makandarasi wala si wazalendo, maana sababu wanazozitoa hazina mashiko na ukizingatia mkataba tulioingia nao muda wake umeishapita kwa hiyo wako nje ya muda," alisema Makilagi.

Diwani wa Isamilo, Charles Nyamasiriri, alisema ujenzi wa choo katika Shule ya Msingi Nyakabungo, ulikuwa umesimama lakini baada ya kuona ujio wa Mkuu wa Wilaya ndio wakaanza tena kujenga.

Meneja Miradi wa MWAUWASA, Gogadi Mgwatu, alisema mkandarasi wa GOPA Contractors Tanzania Limited alipewa mkataba wa kujenga vyoo katika shule 11 wilayani Nyamagana kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5 na CF Builders alipewa mkataba wa kujenga vyoo 12 wenye gharama ya Sh. bilioni 2.2.

Mgwatu alisema mkataba huo wa GOPA Contractors Tanzania Limited ulianza Januari, 2021 na ulitarajia kukamilika Januari, mwaka huu, lakini kutokana na sababu mbalimbali wamemwongezea mkataba wa mwezi mmoja, hivyo wanategemea akamilishe Machi, mwaka huu.

"Kwa ujumla maendeleo ya utekelezaji mradi huo si mazuri. Mkandarasi amekamilisha asilimia 65 tu ya kazi zake zote za mkataba. Tumemwongezea mpaka Machi tunategemea atakuwa amekamilisha ujenzi wa vyoo hivi ili vitumiwe na wanafunzi," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya CF Builders, Ferdinand Chacha, alipoulizwa kwa njia ya simu kuhusu agizo la Mkuu wa Wilaya, alisema hajapokea barua rasmi ya kusimamishwa.

# Rais Mwinyi apigia debe soko la mwani

**Na Mwandishi Wetu**



RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiomba Benki ya AFREXIM kushirikiana na serikali ya Zanzibar katika kupata mchanganuo wa masoko ya mwani, ili wakulima wa zao hilo wanufaike.

Dk. Mwinyi alitoa ombi hilo jana alipokutana na uongozi wa AFREXIM kutoka Misri, uliofika Ikulu jijini Zanzibar ikiwa ni mwendelezo wa mazungumzo yake na serikali kwa lengo kubaini maeneo yenye fursa za uwekezaji nchini.

Alisema kupitia sekta ya kilimo, Zanzibar inategemea mazao makuu mawili ya biashara, likiwamo mwani na wakulima wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kuuza mwani kwa bei ndogo katika masoko.

"Soko la karafuu liko vizuri, tatizo kubwa liko kwenye soko la mwani. Ni eneo ambalo tunahitaji kupata ushirikiano ili kuliongezea thamani zao hilo pamoja na kuinua kiwango cha bei ili wakulima wetu wanufaike," alisema.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar ina maeneo mengi ya uwekezaji kupitia sekta ya uchumi wa bluu, ikihusisha sekta za utalii, mafuta na gesi, uvuvi, hivyo akabainisha umuhimu wa benki hiyo katika kushirikiana na serikali kuziendeleza.

Alisema Zanzibar inakabiliwa na tatizo la miundombinu chakavu isiyokidhi mahitaji ya uhifadhi wa mafuta.

Rais Dk. Mwinyi alipongeza utayari wa benki hiyo katika kuendeleza mazungumzo yatakayofanikisha kuanzishwa kwa ujenzi wa miundombinu ya kituo cha mikutano ya kimataifa na maeneo ya viwanda.

Aliipongeza Benki ya AFREXIM kwa kuwa ina uwezo mkubwa na imekuwa ikishirikiana na serikali barani Afrika katika uwekezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo. Makamu wa Rais Mtendaji, Maendeleo ya Biashara wa AFREXIM, Amri Kamel, alisema uongozi wake utaendelea kuzungumza na taasisi mbalimbali zinazohusika na sekta za uwekezaji na kufanyia kazi ushauri uliotolewa na Rais Mwinyi ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Ujio wa uongozi wa AFREXIM nchini unafuatia ziara iliyofanywa na Rais Dk. Mwinyi mapema mwaka huu nchini Afrika Kusini na kukutana kwa mazungumzo na uongozi wa benki hiyo.

# UNFPA yatoa 'boda' kwa polisi

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi, Dawati la Jinsia na Watoto limepokea pikipiki 10 kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), kwa ajili ya kusaidia operesheni ya kupinga ukatili wa kijinsia, katika wilaya zilizoko Kanda ya Ziwa.

Pikipiki hizo zenye thamani ya shilingi milioni 51.3 zitakwenda wilayani Bunda, Butiama, Serengeti mkoani Mara na Buhigwe, Manyovu, Uvinza katika Mkoa wa Kigoma.

Mwakilishi wa shirika hilo, Georgette Kyomba, alikabidhi pikipiki hizo jana, jijini Dar es Salaam kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Simon Sirro.

Kyomba alisema Tanzania kama ilivyo nchi zingine duniani inakumbwa na matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, na kwamba takwimu zinaonyesha katika 10 wanne walio na umri kuanzia mika 15 hadi 49, hukumbwa na matukio hayo kwenye maisha yao.

Alisema kwamba makabidhiano hayo yamelenga kumlinda mwanamke, mzee na msichana na vitendo vya kikatili ikiwamo ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni pamoja na kufikia malengo ya mpango wa taifa katika kupinga ukatili.

"Asilimia 58 ya wanawake waliofanyiwa ukeketaji ipo mkoani Manyara, ikizidi kiwango cha kitaifa ambacho ni asilimia 10. Katika matukio hayo wamo waliojeruhiwa mioyo yao, familia kuvunjika, jamii na kusababisha kushuka kwa uchumi miongoni mwa jamii," alisema Kyomba na kuongeza:

"Ukeketaji, ndoa za utotoni, mimba na ukatili wa aina nyingine unasababisha ulemavu, vifo na matatizo ya kisaikolojia na kumfanya mtendewa kutofikia maendeleo aliyojiwekea."

Kadhalika, Kyomba alibainisha mkakati wa kufungua madawati matatu mapya ya kijinsia mkoani Manyara na kufanyika ukarabati dawati la Msalala wilayani Shinyanga pamoja na kuimarisha maofisa wa polisi kupata mafunzo ya awali zinazohusu shughuli hizo ili kutoa msaada kwa wakati.

"Kwa kutumia pikipiki hizi waathiriwa wa matukio ya ukatili wa kijinsia watatambuliwa mapema, kulindwa na kusaidiwa na hatimaye kuondoa ukimya kuhusu matukio haya kutokana na mila potofu. Vitendo hivi havikubaliki," alisema Kyomba.

Akizungumza baada kupokea pikipiki hizo, IGP Sirro alisema msaada huo utaongeza wigo wa madawati hayo katika kuwafikia waathiriwa wa matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Tuachane na mila potofu, tunahitaji juhudi za pamoja katika kukomesha ukatili wa kijinsia. Msaada huu utawasaidia maofisa walioko kwenye madawati kuifikia jamii na kutoa elimu. Tunaomba UNFPA pia ifikiri namna ya kuwasaidia polisi ngazi ya kata ili kuongeza kasi ya utolewaji taarifa, huko ndiko kwenye matukio zaidi," alisema Sirro.


EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA: KWA AJILI UTOAJI WA HUDUMA ZA UHAMISHAJI**
**KUMB NA. 10007512**

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Kama sehemu ya ufunguaji wa ofisi katika mkoa wa Dar Es Salaam, EACOP inatafuta watoa huduma za kusaidia shughuli za uhamishaji ofisi. Hivyo, EACOP inayaalika makampuni yenye uzoefu na yenye sifa stahiki kuonesha nia ya utoaji huduma za uhamishaji katika mkoa wa Dar es Salam.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

- Kusaidia kuweka mpango na ratiba ya uhamishaji ofisi.
- Kutoa usaidizi wa dharura wa kitaalamu wa uhamaji ndani ya jengo moja (kama vile toka ghorofa moja hadi jingine).
- Utoaji wa vifaa vya kusaidia katika uhamishaji (mfano vifaa vya kufungashia, maboksi, kamba nk.).
- Kufungasha, kuweka vitu kwenye maboksi na kutoa msaada wakati wa maandalizi.
- Kuhama kutoka jengo moja hadi jingine au ndani ya ofisi.
- Fidia ya bima ya uharibifu kutokana na uhamaji wa vitu au kutoka sehemu moja hadi nyingine
- Uorodheshaji na ufuatiliaji wa vitu vilivyohamishwa.

**VIWANGO VYA USALAMA NA MAHITAJI MENGINE:**

- Mtoa huduma akubaliane na kuthibitisha kwamba waajiriwa wake watatii kanuni za OSHA.
- Mtoa huduma ahakikishe wafanyakazi watatambulika ama kwa sare, vitambulisho, beji au vifaa vingine vya kujilinda kwa ajili ya usalama kwenye eneo la kazi (sehemu zote mbili yaani mahali pa kuhamishwa na pa kuhamishia) na azingatie mahitaji ya usalama wa jengo.
- EACOP haitaruhusu mfanyakazi yeyote ambaye hatakidhi matarajio haya kuingia katika eneo la kazi.
- Mtoa huduma atatakiwa kutoa Vifaa vya kujikinga vinavyohitajika kwa kila mfanyakazi wake (mfano viatu vya usalama, glavu na kofia ngumu pamoja na miwani ya usalama).
- Mtoa huduma atatakiwa kutoa nyenzo za usafilishaji kama vile, malori, matoroli, mikokoteni au vifaa vingine vya kiusalama vinavyohitajika ili kuhamisha vitu vizito.
- Mtoa huduma atachukua tahadhari kwa ajili ya kulinda vitu vinavyosafirishwa dhidi ya kuathiriwa na hali ya hewa (mfano jua, mvua…).

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi yakimbatanisha:

- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha kuthibitisha kulipa kodi kwa mwaka uliopita
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzidata ya EWURA ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kutuma maombi.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani.
- Aoneshe rejea za uzeofu wa huduma alizowahi kufanya zinazofanana na huduma za uhamishaji wa ofisi au vitu.
- Kutoa taarifa ya fedha ya mwaka uliopita

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) kabla ya saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), siku ya tarehe **Machi 3 2022.** Anwani ya Barua pepe sharti iwe na Kumb Na: **00110007512.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa kampuni za awali zenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

216710002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watumishi Afya wanastahili kulipwa posho muda wa ziada

**TUNAWEZA** kusema kwamba watumishi wa afya ni askari wa mstari wa mbele waliopambana katika mazingira magumu ili kuokoa maisha ya Watanzania wenzao muda mfupi baada ya ugonjwa wa UVIKO-19 ulipoingia nchini mwaka 2020.

Ni mazingira magumu kutokana na ukweli kwamba wakati ugonjwa unaingia nchini, hawakuwa na vifaa vya kutosha vya kuwakinga wao, hivyo tunaamini kuwa walijitoa kuhakikisha UVIKO-19 hausambai kwa kasi nchini. Hakika walitekeleza wajibu wao ipasavyo licha ya kipindi hicho kuwa cha tishio, kutokana na wenzao wengi katika mataifa mengine walivyokuwa wakipoteza maisha.

Kama ambavyo wataalamu wa afya wamekuwa wakielezewa kuwa adui UVIKO-19 haonekani na wakati mwingine anasababisha vifo na kwamba kazi ya kukabiliana na janga hilo ni ngumu. Kwa kutambua ugumu wa kazi hiyo, serikali imesema inapanga kulipa madeni na stahiki zilizosalia za wazabuni na watumishi, zikiwamo posho ya saa za ziada kwa waliofanya kazi ya kuokoa maisha ya Watanzania wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo. Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), maelekezo yametolewa kwa Mamlaka za Mikoa na Halmashauri kuandaa madai yote ya posho za saa za ziada wanazodai watumishi wa afya waliofanya kazi usiku na mchana katika mapambano ya kukabiliana na janga la ugonjwa wa UVIKO-19.

Kauli hiyo ya serikali ilitolewa bungeni juzi TAMISEMI ilipokuwa ikijibu swali la mmoja wa wabunge, na kubainisha jinsi watumishi wa sekta hiyo walivyotimiza wajimu wao katika mazingira magumu na yenye tishio kubwa wakati ule.

Tunaunga mkono uamuzi huo, kutokana na ukweli kwamba watumishi hao walifanya kazi kubwa katika mazingira magumu ya kutokuwa na vifaa vya kujikinga na ugonjwa kwa lengo la kuokoa maisha ya Watanzania wenzao. Hatua ya serikali kuamua kulipa madeni yote ya posho za ziada wanazodai watumishi wa afya, tunadhani kwamba zinaweza kuwafanya wawe na ari na moyo wa kutimiza majukumu yao bila manung'uniko. Vilevile, hatua hiyo tunaamini inaonyesha ni jinsi gani serikali inavyotambua mchango wao, kwa jinsi walivyojitoa kwa hali na mali na bila kuhofia maisha yao binafsi, hivyo kutanguliza mbele maslahi mapana ya taifa. Wakati wa mlipuko wa ugonjwa nchini, ni wazi watumishi wa afya walifanya kazi kubwa usiku na mchana katika mapambano ya kukabiliana na janga hilo ambalo linaendelea kuumiza dunia.


Kitendo cha serikali kutambua mchango huo na kuahidi kulipa mabaki ya posho, tunaamini kinaonyesha ni jinsi gani inatambua, inajali na kuthamini mchango wa wataalamu hao wa afya kwa maisha ya Watanzania. Madaktari, wauguzi, walezi na huduma za matibabu nchini, kama walivyo wenzao ulimwenguni walikabiliwa na mzigo mkubwa katika majukumu yao, hivyo tunaona hatua ya kukumbuka masalia yao ni jambo la muhimu. Lakini tunawashauri watumishi wa afya kutokata tamaa wanapokumbana na vikwazo mbalimbali wakati wa kutekeleza majukumu yao, bali waendelee na moyo huo waliouonyesha ugonjwa huo ulipoingia nchini.

Hawakuwa na vifaa vya kutosha kwa ajili ya usalama wao wanapohudumia wagonjwa wa UVIKO-19, lakini hawakata tamaa, hivyo tunadiriki kuwafananisha na wanajeshi wanavyojitoa mhanga kuhakikisha wanapoteza hata maisha yao lengo likiwa kulinda mipaka na uhuru wa nchi yao. Ukweli ni kwamba, kufanya kazi katika mazingira hayo ambayo hayana vifaa au dawa, ni hatari, lakini wao wamemudu mazingira hayo hatarishi kwa lengo la kuokoa maisha ya Watanzania, tunadhani hawanabudi kupata haki zao.

Ni kweli kwamba stahiki hizo zimechelewa kutolewa, lakini hali hiyo inatokana na hali halisi ya uwezo mdogo wa serikali katika kugharimia mambo mengi. Hatua ya serikali kupanga kulipa masalia ya watumishi hao inaonyesha jinsi gani ilivyo na dhamira ya dhati ya kuwalipa kwa kutambua kazi yao nzuri ya utumishi uliotukuka.

Tunaelewa kwamba katika miaka ya karibuni, serikali ilifuta posho za ziada kwa watumishi wa umma kwa kutumia sheria, lakini hilo hatuamini kama litakwamisha nia hiyo njema ya kutambua kazi yao nzuri na kuwaenzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Litafutwe suluhisho la kudumu kukomesha mikasa moto sokoni

Na Adam Fungamwango

**USIKU** wa kuamkia Februari 13, moto mkubwa ulizuka kwenye soko la wafanyabiashara maarufu kama 'wamachinga' eneo la Mbagala Rangitatu, jijini Dar es Salaam.

Sehemu iliyoathirika zaidi ni wauza nguo za mitumba ambayo baadhi ya bidhaa ziliteketea. Tumshukuru Muumba hakuna ripoti za vifo.

Ajali hiyo ya moto imetokea ikiwa imepita takriban mwezi mmoja tangu kuungua Soko la Karume, Dar es Salaam hata kuteketezwa vibanda mali ya wafanyabiashara.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, Jumapili iliyopita mbali na kuthibitisha tukio, akaunda tume kuchunguza akiipatia siku nne iwe imekamilisha uchunguzi huo, ambayo ilitarajiwa juzi ripoti yake kuwasilishwa kwa aliyeunda.

Hiyo si mara ya kwanza soko la Mbagala Rangi Tatu kuungua, kwani Machi 6, mwaka 2018, soko hilo liliwahi kushika moto.

Ni usiku na kuamkia Januari 16, Soko la Karume lililoko Ilala Mchikichini, nalo liliungua na kuharibu mali nyingi za wafanyabiashara zaidi ya 3,500, ikiambatana na hasara kubwa. Nako Mwenyezi, ashukuriwe hakuna kifo kilichoripotiwa.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliunda tume kwa majibu yaliyotoka, chanzo ni vijana wa wasio na maadili maarufu 'mateja' ndiyo walisababisha ajali hiyo kwa kuwasha mshumaa walioutelekeza bila ya kuuzima.

Julai 11, mwaka jana, soko kubwa si Tanzania tu, bali la Afrika Mashariki na Kati, Kariakoo jijini Dar es Salaam na likateketea kwa moto uliozuka kuanzia saa tatu usiku.

Ingawa chanzo hakijajulikana, lakini ulidaiwa kuanza kwenye paa la juu la soko hilo na baadaye kusambaa kwenye maeneo mengine.

Hapa nimeorodhesha ajali za moto kwenye masoko ambayo kwa siku za karibuni, zimekuwa zikiibuka na kuacha maswali mengi kwa Watanzania.

Ingawa si mara ya kwanza kuwapo ajali mbalimbali za moto sehemu mbalimbali, ikiwamo kwenye masoko, hata mwaka 2017 soko la Sido Mbeya liliungua moto.

Sasa, umefika wakati wa kujiuliza kwa kina na kutafakari,

sababu za masoko hayo kuungua, hasa kwa siku za karibuni.

Tuwapongeze viongozi wa serikali kwamba wamekuwa karibu na wananchi pamoja na waathirika wote wa majanga, ikiwa ni pamoja na kuunda tume. Niseme, umefika wakati hizi tume baada ya kutoa ripoti zao, ziende mbali zaidi na kutafuta suluhisho la kudumu, maana inaonekana kuwapo dalili za matukio kuwa endelevu.

Tume ikija na majibu ni 'mateja' waliochoma isiishie hapo, bali hatua zaidi inahitajika. Nitapenda, ikiletwa majibu kuwa ni hitilafu ya umeme au kinamama walikuwa wameacha majiko ya mkaa yakiwa yanawaka, halafu ikaishia hapo, bado tatizo linaweza kuendelea kwingine.

Ni sawa na mzazi kufanya uchunguzi na kugundua mtoto wake amefariki na ugonjwa malaria, halafu ikaishia hapo bila kuanza kununua chandarua, kupuliza dawa na vitu vingine zitakavyosababisha mbu wasikaribie nyumba yake, badala ya kusubiri tena mwingine augue au afe, ili afanye uchunguzi mwingine.

Tusisubiri masoko mengine yaungue ili kuunda tena tume zingine. Matokeo ya tume zote yaangaliwe, na vyanzo zitakavyonekana ndiyo sababu kuu ya masoko kuungua, basi kazi ifanyike ili kuzua moto usitokee tena.

Kama ni mateja, basi mkakati ufanywe kuongeza walinzi masokoni, ili kutoruhsu mtu yoyote kusogelea maeneo hayo hasa linapokuwa limefungwa. Kama ni hitilafu ya umeme basi mifumo yote ya umeme kwenye masoko yote nchini yaangaliwe upya.

Yafumuliwe na kuanza kutandaza upya kisasa zaidi. Kama ni hujuma, basi nadhani wana usalama wetu wanajua nini la kufanya. Hii ndiyo maana ya tume ambazo viongozi wetu wanapendekeza. Wanataka sababu ikipatikana, basi wanaohusika sasa wafanyie kazi ili kuzuia lisitokee tena.

Hapa ni suala la uwajibikaji pamoja. Lisiachwe kwa viongozi tu, bali hata kada zingine kama wanausalama wote wakiwamo askari Polisi, Zimamoto na Uokoaji, na hata wadau wa umeme -Tanesco. Niseme tu, kinga ni bora kuliko tiba.

# HABARI PICHANI



Meneja wa Kiwanda cha Uchapaji Magazeti cha The Guardian Ltd, Balasubramaniyan Venkadachalam (kushoto), akimwonyesha Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Sitholizwe Mdlalose, jinsi gazeti linavyochapishwa wakati alipotembelea vyombo vya habari vya IPP jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa The Guardian Ltd, Joyce Luhanga.



Meneja wa East Africa Radio, Lydia Igarabuza, akimwelezea Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom, Sitholizwe Mdlalose, jinsi vipindi vya redio vinavyorushwa.

**PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania, Sitholizwe Mdlalose (katikati), akicheza muziki ndani ya studio za radio za EAST Africa radio jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano wa Vodacom, Rosalyn Mworia.



Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile, akimwonyesha Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom, Sitholizwe Mdlalose, namna vipindi vinavyorushwa alipotembelea Radio One jana.




Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom, Sitholizwe Mdlalose, akiwa katika studio ya kurushia taarifa ya habari ya ITV jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Vipindi wa ITV, Pius Paul.



Mkurugenzi wa Vodacom, Sitholizwe Mdlalose (mwenye suti), akizungumza na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallece Mauggo, alipotembelea kiwanda cha uchapaji magazeti ya kampuni ya The Guardian Ltd jana. Kulia ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Joyce Luhanga.

# TANAPA yatakiwa kuongeza juhudi kujitangaza

**Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wadhamini wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Jenerali (mstaafu) George Waitara, amelitaka shirika hilo kuongeza juhudi zaidi kutangaza vivutio na fursa za uwekezaji.

Jenerali Waitara amesema hatua hiyo itaongeza wigo wa watalii kutembelea hifadhi hizo na kuchangia pato la taifa.

Waitara aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa ziara ya bodi ya wadhamini katika Hifadhi ya Taifa ya Saadani kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli za maendeleo na changamoto zinazoikabili na namna bora ya kuzitatua.

"Mnafanya vizuri katika kutangaza vivutio vya utalii. Nataka mwongeze juhudi zaidi za kuzitangaza hifadhi na vivutio vyake," alisema Waitara.

Awali, Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, William Mwakilema, aliwashukuru wajumbe wa bodi kwa kutenga muda wao na kuitembelea hifadhi hiyo na kujionea shughuli za maendeleo zinazofanyika katika eneo hilo pamoja na changamoto zake ili kuzipatia ufumbuzi.

Pia Mwakilema alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kushiriki kutangaza utalii kupitia kampeni ya "Royal Tour" pamoja na kuelekeza fedha nyingi kwenye shughuli za kuimarisha utalii nchini.

"Tunashukuru juhudi za Rais wetu ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu kwa kuleta fedha nyingi kwenye hifadhi zetu. Lengo lake ni kuona namna ambavyo sekta hii inaimarika na kuchangia pato la taifa," alisema Mwakilema.

Naye Kamishna wa Uhifadhi Kanda ya Mashariki, Steria Ndaga, alisema mikakati mbalimbali ya kukuza utalii katika kanda hiyo imewekwa ikiwamo uboreshaji wa miundombinu kupitia fedha za UVIKO -19. Alisema Sh. bilioni moja itatumika kukarabati miundombinu ya uwanja wa ndege, madaraja, vyoo na barabara ili kuboresha huduma zinazopatikana kwenye hifadhi.

Pia Kamishna Ndaga alibainisha kuimarika kwa ushirikiano baina ya hifadhi hiyo na waongoza watalii kutoka Zanzibar na kwamba zaidi ya kampuni 30 zinatarajiwa kutembelea na kujionea vivutio vilivyomo ndani ya hifadhi kwa lengo la kuendelea kuitangaza Hifadhi ya Saadani kwa wageni wanaotembelea Zanzibar. Akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo mbele ya bodi ya wadhamini, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Saadani, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Ephraim Mwangomo, alibainisha fursa mbalimbali za uwekezaji zinazopatikana kwenye hifadhi hiyo ikiwa ni pamoja na soko la uhakika la wageni kutoka miji inayoizunguka hifadhi hii ikiwamo Zanzibar.

Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini walipata fursa ya kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa ikiwamo uboreshaji wa miundombinu ya barabara, uwanja wa ndege, utalii wa boti na kiwanja cha mchezo wa gofu.



Dk. Judith Mwijage kutoka Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam akizungumza na wasichana wa Shule ya Sekondari ya Zanaki kuhusu vikwazo alivyopitia katika safari yake ya kuutafuta udaktari na jinsi alivyokabiliana navyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kunenge ataka taasisi za umma kutambua vipaumbele vya serikali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema taasisi wezeshi zilizoko katika mkoa zinatakiwa kutambua vipaumbele vya serikali ili kufanikisha ukuaji wa uchumi kupitia uwekezaji wa viwanda.

Kunenge aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa wafanyabiashara mkoani Pwani uliohudhuriwa pia na taasisi wezeshi. Taasisi hizo ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA,) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salam (DAWASA) na Malmlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kunenge alisema kila taasisi inatakiwa kufanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria ili kufanikisha ukuaji wa pato la taifa kwa mkoa.

Alisema vikwazo katika taasisi wezeshi vinaendelea kututuliwa na kwamba kwa sasa katika eneo la viwanda la Zegereni, Kibaha, kuna barabara ya lami yenye urefu wa kilometa 12 .5 inayoendelea kujengwa ili kuwezesha urahisi katika usafirishaji wa bidhaa na mali ghafi.

Pia alisema mkoa tayari umeanzisha kituo cha pamoja ambapo taasisi wezeshi 15 zitakuwa hapo kwa ajili ya kututua vikwazo vya wawekezaji na kutoa maelezo kwa wanaotaka kufanya uwekezaji.

Kuhusu suala la maji, Kunenge alisema kuna mradi wa usambazaji wa maji kutoka bwawa la Mwalimu Nyerere, Rufiji kwenda katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambao utaondoa upungufu wa huduma hiyo kwenye maeneo ya mkoa husuan ya viwanda na wananchi.

Mkuu huyo wa mkoa alisema anashangazwa na mchango wa pato la taifa wa asilimia 1.95 wakati mkoa huo unaongoza kwa uwekezaji wa viwanda.

"Hii asilimia 1.95 ambayo mkoa unachangia kwenye pato la taifa haiendani na hali halisi. Mkoa una viwanda vingi kwa nini mchango wetu uwe mdogo? alihoji.

Kunenge alisema endapo kila mmoja atasimamia vizuri katika nafasi yake, uchumi wa mkoa utakua na mchango wa pato la taifa utaongezeka.

Mhandisi Miradi na Miundombinu wa DAWASA, Yohana Msangula, alisema uhaba wa maji katika eneo la viwanda Zegereni unaendelea kupatiwa ufumbuzi na kwamba hivi sasa kuna mradi unatekelezwa na ulazaji wa mabomba unaendelea.

# 90% wafanyakazi wa shirika wapata chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Kiota Women Health and Development Organization (KIWOHEDE), limesema asilimia 90 ya wafanyakazi wake wamepata chanjo ya UVIKO-19, tangu ilipoanza kutolewa mwaka jana.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Justa Mwaituka, alipokuwa akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa wanafanya hivyo kwa kuwa chanjo ni ya muhimu.

KIWOHEDE ina wafanyakazi 50 nchi nzima, na tayari asilimia 90 wameshapata chanjo, nikiwamo mimi kiongozi wao ambaye nilikuwa wa kwanza chanjo zilipoanza kutolewa," alisema Mwaituka.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema, shirika lake limefikia mafanikio hayo ya watumishi wake wengi kupata chanjo kutokana na kwamba wamehamasishana na kuelewa umuhimu wa kujikinga na ugonjwa huo.

"Lakini mimi kiongozi wao nilikuwa mtu wa kwanza kuchanjwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuzindua chanjo, na wengine nao wakahamasika na kujitokeza kuchanjwa hadi wamefikia asilimia 90," alisema.

Mwaituka alisema, watumishi wa KIWOHEDE hawakusubiri kuhamasishwa na watu wa afya, bali walihamasishana wenyewe, kwa kuwa wanajua madhara ya ugonjwa huo na umuhimu wa chanjo.

"Kwa kuwa asilimia kubwa ya wafanyakazi wetu wamechanjwa na nina uhakika wachache waliosalia nao watachanjwa, kwani tunaendelea kuelimishana, hasa kwa kuzingatia kwamba suala hili ni la hiari," alisema.

Aidha, alisema si kuchanja tu bali wanaendelea kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Afya ikiwamo kunawa maji tiririka, sabuni, vitakasa mikono lakini pia watumishi na wageni wanaofika ofisi za shirika hilo kuvaa barakoa.

"Nitoe wito kwa Watanzania wenzangu kwamba, tuachane na elimu za mitaani zinazopingana na za wataalamu wa afya, kwani corona ipo na inaendelea kuangamiza maisha ya watu. Tuchukue tahadhari," alisema.

Alisema tangu ugonjwa huo ulipoingia nchini mwaka 2020, kumekuwapo na elimu inayokwenda kinyume na maelekezo ya wataalamu wa afya, na kwamba hali hiyo inasababisha baadhi ya watu wasijitokeze kuchanjwa.

HABARI KITAIFA

# Wanawake wapewa siri kuwa viongozi

Na Mwandishi Wetu

WANAWAKE wamedokezwa juu ya umuhimu wa kukuza vipaji vyao vya uongozi katika zama hizi za kampuni kubwa na kufanya kazi kwa pamoja katika mashirika.

Hayo yalisemwa kwenye tukio maalumu lililoandaliwa na kampuni ya SGA Security, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Wapendanao, ambapo wafanyakazi wanawake 6,000 nchini walipokea ukufunzi maalumu juu ya uongozi na namna ya kukabili hisia kwa njia chanya.

Tukio hilo liliwezeshwa na mzungumzaji George Obado, ambaye ni mtaalamu kwenye masuala ya uongozi na Ruth Serem, mtaalamu katika masuala ya uwezeshaji wanawake, akiwapitisha wanawake katika hatua mbalimbali na sifa za kile wataalamu wanachoita 'mwanamke asiye wa kawaida'. Kundi la wawakilishi kutoka sehemu mbalimbali za SGA lilidokeza juu ya namna ya kukabili hisia, ikiwa ni somo la wakati huu kwa viongozi kwenye dunia ya leo ya kampuni kubwa.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Tanzania, Eric Sambu, alirejea kwamba wanawake wanahusika kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa uamuzi wa kimkakati.

Alieleza jinsi wanawake walivyo na zawadi ya kiasili katika kusimamia na kutatua hali mbaya na mara nyingi hufikiria sababu zote zinazoweza kuathiri lengi na hivyo wakati mwingi huwa sawa katika waamuayo na kufanya.

Aliwahimiza wanawake kujiamini na kutumia faida za zawadi zao za asili kujipandisha wenyewe kwenye nafasi za ushawishi kwenye ulimwengu huu wa ushirikiano. Aliwashauri dhidi ya kuwaona wenzao kana kwamba wapinzani, badala yake wajielekeze kwenye kutwaa kinachopatikana kwenye kujuana kwao na kufanya kazi pamoja.

George Obado alirejea juu ya haja kwa wanawake kujitambua, kudhibiti na kuhamasishana wenyewe na kumudu vyema uhusiano, wakitazama pia wajibu wao kijamii. Aliwashauri wawe na tunu binafsi na kumudu vyema na kiutu uzima mihemko na ili kufanya hayo, wanatakiwa kuelewa juu ya nguvu na udhaifu wao.

Ruth Serem naye alitoa vidokezo juu ya jinsi ya kuwa mwanamke wa kitofauti au asiye wa kawaida, akachukua kile alichiopata kusema Maya Abgtelou, kwamba wamefanywa kuwa maalumu, na kwa hakika si watu wa kawaida.

Meneja Rasilimaliwatu wa SGA Security, Ebenezer Kaale, alisema kwamba kampuni hiyo inawapa moyo wanaume katika nafasi zao kuendelea na ustawi, akisema ndiyo siri ya mafanikio yao.

"Japokuwa sekta ya usalama haijavuta wanawake wengi, SGA imejenga mazingira sawa na inao wanawake wengi kwenye safu muhimu na uzoefu unaonesha kwamba wamekuwa si wa kawaida," alisema. "Wanawake ni waangalifu zaidi huku wakifuata sera na kanuni zilizowekwa na kwa mara nyingi ni waaminifu, na hizi ndizo sifa muhimu kwenye sekta hii," aliongeza.



Sehemu ya waajiriwa wanawake wa kampuni ya SGA Security wakisherehekea Siku ya Wapendanao Jumatatu iliyopita. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Tanzania, Eric Sambu na mzungumzaji mtoa motisha, George Obado. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wafanyabiashara washauriwa bima

Na Mwandishi Wetu, KATAVI

WAFANYABIASHARA mkoani Katavi wametakiwa kukata bima kwa ajili ya kulinda biashara zao wakati wanapokabiliwa na majanga mbalimbali ukiwamo moto.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, aliyasema hayo juzi alipowatembelea wafanyabiashara wanaomiliki viwanda vya kuchakata mchele, karanga na alizeti ili kijionea ukarabati wa majengo ya kuhifadhia bidhaa yaliyoezuliwa na upepo mkali uliotokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika eneo la Maji moto lililoko Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe mkoani humo.

Pinda alisema kuwa faida kubwa watakayoipata wafanyabiashara hao ni kutosimamisha huduma zao kwa muda mrefu kwa kuwa pindi majanga yatakapotokea kampuni husika zitawalipa fidia.

"Nawahimiza kukata bima, kwa sababu ukiwa na bima kwenye mradi wako unakuwa hauna cha kuhofia wakati wa kuendesha shughuli zako hata likitokea la kutokea kampuni za bima zitakulipa ndani ya muda mfupi, hatua itakayosaidia kuendelea na uzalishaji bila wasiwasi," alisema.

Aliahidi kushughulikia kero zinazowakabili wafanyabiashara wa viwandani ikiwamo tatizo la umeme ambao umekuwa ukikatika mara kwa mara na kukwamisha uzalishaji.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wenzake, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Flamingo Foods, Leonard Lusaganya, aliishukuru Serikali ya Mkoa wa Katavi kwa kuboresha mazingira mazuri ya uwekezaji ambayo yamesaidia kuongeza uzalishaji kwa kiwango kikubwa.

## Bunge laja na ushauri kukatika kwa umeme

Na Salome Kitomari, DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, imetoa ushauri kwenye maeneo manane ili kuliwezesha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), huku ikieleza kuwa hakuna sababu za msingi za kukatika katika umeme.

Kadhalika imetaka wizara kufanya tathmini ya hasara za kiuchumi kwa nchi kutokana na kukatika kwa umeme mara kwa mara na kuchukua hatua stahiki kama kamati ilivyoelekeza ili kuepuka athari za kiuchumi ambazo nchi inazipata.

"Hii itasaidia kujua athari za uchumi kwa nchi, na TANESCO kuondokana na utendaji wa mazoea,"alisema Danstan Kitandula, Mwenyekiti wa Kamati hiyo akiwasilisha taarifa jana.

Alisema ni muhimu TANESCO ipewe fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika mwaka huu wa fedha, ili iweze kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu yake na kuondoa tatizo la umeme kukatika mara kwa mara.

Pia, alisema iongezewe bajeti kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili iweze kukarabati miundombinu hiyo na kuondoa tatizo la umeme kukatika mara kwa mara.

Aidha, alisema serikali iandae mkakati wa kudhibiti upotevu na wizi wa umeme sambamba na kudhibiti upotevu wa mapato yake.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wa umeme nchini shirika hilo lifunge vifaa vyenye uwezo wa kusambaza umeme kwa wateja wengi, ikiwamo kufunga mashine nyumba zenye uwezo wa kuhudumia wateja kadiri ya mahitaji yao.

"Serikali itoe tamko na elimu kwa wananchi juu ya gharama za kuunganishiwa umeme ili kuondoa mkanganyiko uliopo na kuongeza uelewa kwa wananchi. Vilevile ni muhimu bei ya umeme iangaliwe ili iwe huduma yenye kuleta ahueni kwa wananchi," alisema.

Pia, alitaka serikali iangalie ubora na uhakika wa umeme wake ili wateja wengi waweze kutumia hususani viwanda vikubwa na ikibidi wawena laini zao mahsusi ili TANESCO ipate mapato ya kutosha.

"Ipo haja kwa serikali kufanya tathmini ya kina kuhusu gharama kubwa inazozitumia TANESCO katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme," alisema na kuongeza:

"Matokeo ya thathmini hiyo yatumike kuijengea TANESCO uwezo kifedha, ili hatimaye iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi."

# Wenye ulemavu 312 wapata ajira serikalini miaka minne

BUNGE limeelezwa kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 serikali imeajiri watumishi wenye ulemavu wapatao 312 wenye sifa stahiki katika fani mbalimbali.

Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) ilibainisha hayo bungeni jana ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya.

Katika swali lake, Manyanya alihoji katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2021 ni walemavu wangapi wenye sifa husika wameajiriwa katika nafasi zilizotolewa na serikali. "Je, hiyo ni sawa na asilimia ngapi ya watu wenye ulemavu wenye sifa hizo nchini," alihoji.

Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema kwa mujibu wa takwimu zilizoko za wahitimu wenye ulemavu ambao wamejiorodhesha katika kanzidata ya serikali inaonyesha kwamba, kuanzia 2018 hadi 2021 wahitimu wenye ulemavu walioajiriwa katika utumishi wa umma ni asilimia 56 ya wahitimu walioko.

Ilitoa rai na kusisitiza wahitimu wenye ulemavu wenye sifa za elimu na taaluma mbalimbali ambazo zipo ndani ya utumishi wa umma kuomba kazi pindi zinapotangazwa ili kuajiriwa katika utumishi wa umma.

Ilisema ajira hutolewa kwa usawa na kwa watu wote wenye sifa zinazohitajika katika nafasi husika pamoja na kuzingatia ujumuishaji wa watu wenye ulemavu.

Vile vile, iliwataka waajiri wote kuzingatia ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu katika ajira zote zinazotangazwa na serikali kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu namba tisa ya Mwaka 2010.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, George Mkuchika, bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Bandari kavu ya Isaka yapigiwa debe kwa wateja

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na Shirika la Reli (TRC), inaendelea kufanya ushawishi kwa wateja wa bandari na wasafirishaji wakiwamo wa nchi za Rwanda, Congo na Burundi kutumia zaidi Bandari kavu ya Isaka.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ilibainisha hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Santiel Kirumba.


Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itaboresha Bandari kavu ya Isaka.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema serikali kupitia TPA, imenunua na kupeleka vifaa vya kuhudumia mizigo ambavyo ni 'forklift' moja na 'reachstaker' moja ambavyo vinatumiwa na TRC kuendesha Bandari Kavu ya Isaka, Shinyanga kwa sasa.

Ilisema lengo la kununua na kupeleka vifaa hivyo katika Bandari kavu ya Isaka ni kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za usafirishaji mizigo kati ya Dar es Salaam, mikoa ya jirani na Shinyanga na nchi jirani za Rwanda, Congo na Burundi.

Ilisema bandari hiyo imekuwa ikitumika kwa kiwango kidogo kutokana na tatizo la mabehewa ya kubeba makasha na injini inayoikabili TRC.

Hata hivyo, ilisema Desemba 2021, TRC imepokea mabehewa 44 na injini tatu za treni kwa ajili ya kuhudumia mizigo kati ya Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu ya Isaka.




Habari zote na Augusta Njoji

# Hati kimila zahojiwa mfuko wa pembejeo

MBUNGE wa Mbozi (CCM), George Mwenisongole, ametaka kujua sababu za mfuko wa pembejeo kutopokea hati za kimila.

Akiuliza swali bungeni leo, alisema mfuko huo ulianzishwa kwa lengo la kusaidia wakulima wadogo walioko vijijini lakini haupokei hati hizo ambazo ndizo zilizoko vijijini.

Wizara ya Kilimo ikitoa ufafanuzi kwenye swali hilo, ilisema mwaka 2005 hadi 2010, mfuko wa pembejeo uliwahi kupokea hati za kimila kama dhamana kwa majaribio ambapo Wilaya ya Mbozi ndiyo ilikuwa eneo la majaribio.

Ilisema baada ya kutoa mikopo hiyo mfuko wa pembejeo ulikabiliwa na tatizo la mikopo kutofanyiwa marejesho.

Aidha, ilisema mfuko wa pembejeo ulipojaribu kuuza mashamba hayo ilishindikana kwa ajili ya kufidia mikopo iliyotolewa haukufanikiwa kutokana na mashamba hayo kuwa ya jamii au ukoo unaoishi pamoja na sio la yule mwenye hati.

Ilibainisha kuwa katika Wilaya ya Mbozi, mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 480.4 kwa wakulima 28 kati ya fedha hizo Sh. milioni 135.9 zilirejeshwa na Sh. milioni 344.5 bado hazijarejeshwa.

Kutokana na kero iliyojitokeza, wizara ilisema Bodi ya Wadhamini mwaka 2016 ilisitisha utoaji wa mikopo kwa kutumia hati hizo kama dhamana mpaka hapo zitakapofanyiwa marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji ili kuondoa tatizo hilo.

## TAMISEMI yachambua maombi ya wilaya mpya

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema inaendelea na uchambuzi wa mapendekezo ya kuanzisha Wilaya ya Bujora na maeneo mengine ya utawala yaliyowasilishwa.


Ofisi hiyo iliyasema hayo jana bungeni katika swali la Mbunge wa Magu (CCM), Boniventura Kiswaga.

Katika swali lake, Kiswaga alihoji lini serikali itatekeleza ahadi ya kuanzisha Wilaya mpya ya Kisesa mkoani Mwanza.

Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema Mkoa wa Mwanza uliwasilisha mapendekezo ya kuanzisha Wilaya ya Bujora (Kisesa) kupitia barua yenye Kumb. Na CFA.77/193/01/62 ya tarehe 15/03/2021 na Kumb. Na. CDA.33/295/01/06 ya tarehe 10/05/2021.


Ilisema inaendelea na uchambuzi huo na utakapokamilika timu ya wataalamu itatumwa kufanya uhakiki na baadaye kuishauri mamlaka ipasavyo juu ya suala hilo.

Ilimshauri mbunge na wananchi wawe na subira katika kipindi ambacho serikali inaendelea na uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa.




Ukurasa 12

**Yanayowasibu walezi wa watoto vichwa vikubwa na mgongo wazi**



Ukurasa 13

...Yajue yanayokaribisha maradhi figo



Ukurasa 14

**MSITU MPYA MABWEPANDE....**

**TAWA ilivyojikita kubadili Pori la Akiba Pande lisibaki kisiwa**

# Waziri Ummy: Mlo wetu unatuongezea maradhi ya saratani kila kunavyokucha

**Na Yasmine Protace**

KUNA vyanzo vingi vya magonjwa nchini; aina ya mlo na mfumo wake zimo katika hesabu. Sasa wanazuoni wa afya wana maoni kwamba, kuna umuhimu wa pekee kufuatwa taratibu sahihi za mlo ili kujiepusha na kupata magonjwa.

Inaelezwa kitaifa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, sasa nchi imepata ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani katika hali inayochangiwa sana na mtindo wa maisha, kutozingatia kanuni sahihi za lishe, pia kutokufanya mazoezi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, hivi karibuni katika maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani, anataja sababu nyinginezo, ni mwili mnene sana, matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, pombe kupita kiasi na ulaji usiofaa wa mboga na matunda, chumvi na sukari kwa wingi.



Watu wakiwa kwenye mjumuiko wa mlo. **PICHA: MTANDAO**

Waziri Ummy anasema katika changamoto hiyo, serikali imeimarisha huduma za kibingwa katika hospitali za Rufani za Kanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili, kwa ajili ya uchunguzi na tiba, ikiwaongezea wataalamu, miundombinu stahiki na vifaa tiba.

"Takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Tafiti za Saratani (IARC) za 2018, zinaonyesha kuwapo wagonjwa wapya 42,060 kwa mwaka na takribani wagonjwa 28,610 sawa na asilimia 68 hufariki kutokana na ugonjwa huo," anasema.

Waziri Ummy anataja wastani katika kila watu 100,000 wanaogundulika, kati yao wanakuwapo 76 wanaogundulika na maradhi ya saratani, ugonjwa unaoathiri watu wa rika na jinsia zote watoto, watu wazima, wanawake na wanaume.

Anafafanua kuwa, katika taarifa za mwaka 2021 kutoka Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, inaonyesha saratani zinazoathiri wanawake takwinu zake katika mabano: Mlango wa Kizazi (43%), Matiti (14.2%) na Koo (3.8%) .

Pia, kwa wanaume anataja mjumuisho huo wa kitakwimu na aina ya kansa ni katika maeneo:Tezi Dume (21%), Koo (11.8%), Utumbo Mkubwa na Mdogo (9%) na ya Mdomo na Kinywa (7.3%).

### ILIVYO KIMATAIFA

Waziri Ummy anarejea takwimu za mwaka 2018 za Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Saratani na Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kila mwaka duniani kote kuna wagonjwa wapya wanaokadiriwa milioni 18.1.

Anasema kati yao, zaidi ya wagonjwa milioni 9.6 ambao wastani wao ni nusu wanafariki kila mwaka, vilevile kukiwapo watu milioni 43.8 wanaoishi nao duniani.

"Kama hatua madhubuti za kinga, uchunguzi wa mapema na tiba stahiki hazitachukuliwa haraka, tatizo la saratani linakadiriwa kuongezeka na idadi ya wagonjwa wapya kufikia milioni 24 ifikapo mwaka 2035, huku ongezeko kubwa likiwa katika ukanda wa nchi zinazoendelea kama Tanzania," anasimulia Waziri Ummy.

Vilevile anaeleza takwimu za kimataifa zinaonyesha kuna wagonjwa wapya 14,136 waliofikiwa na huduma hiyo, sawa na asilimia 33 ya makadirio ya wagonjwa wapya wote mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia tano, kwani mwaka jana ilikuwa asilimia 28 sawa na wagonjwa 12,096.

### KINACHOIPONZA JAMII

"Ongezeko la wagonjwa wa saratani pamoja na magonjwa mengine yasiyoambukiza yanachangiwa zaidi na mtindo wa maisha usiozingatia afya bora kama kutokufanya mazoezi (Tabia Bwete)," anatamka na kuendelea:

"Unene uliokithiri, matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, matumizi ya pombe kupita kiasi na ulaji usiofaa kama kutokula mbogamboga na matunda, matumizi ya chumvi na sukari kwa wingi."

Waziri Ummy anasema katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Tanzania imeshuhudia ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani inayochangiwa na mtindo wa maisha, ikilinganishwa na ilivyokuwa awali, wengi walikuwa wenye saratani zinazotokana na maambukizi ya virusi.

"Ni vyema kila mmoja akapima afya yake mara kwa mara ili kutambua hali yake ya kiafya. Endapo utatambuliwa kuwa una ugonjwa wa saratani, tumia huduma za afya kulingana na ushauri utakaopewa na wataalamu wa afya," anasema.

Pia, anafafanua kwa watakaojitambua kuwa na saratani muhimu ni kutumia ipasavyo huduma za afya kwa manufaa ya afya yao na kujiepusha na athari zake, hasa kwa wasiotumia vyema huduma za kiafya.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, Tanzania imetunga sheria, miongozo na mikakati ya udhibiti wa vihatarishi, ili kuwezesha kudhibiti ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza, akiwarejea wataalamu kwamba theluthi moja zinatibika.

• **Soma zaidi uk 13 chini.**

AFYA

MAISHA NI MTIHANI...

# Yanayowasibu walezi wa watoto vichwa vikubwa na mgongo wazi



Kinamama wenye watoto wenye vichwa vikubwa wakipata matibabu hospitalini. **PICHA: MAKTABA**

**Na Christina Mwakangale**

MAMA Nancy (si jina halisi) anaishi Buguruni jijini Dar es Salaam. Umbali wa kutoka kituo cha daladala Buguruni-Rosana hadi anakoishi Mama Nancy ni mita 20, alikopanga vyumba viwili.

Anapokuwa nyumbani sebuleni ni vigumu kubaini iwapo ana mtoto ndani, kwani ni patulivu. Kumbe kando yake amekaa Nancy, anayeangalia picha za watoto kwenye televisheni.

Kwa kumtazama Nancy (8), si kama watoto wengine wa umri wake. Hata mgeni anapoingia mazingira ya nyumbani kwao, ni vigumu kuamkia au hata kumkaribisha mgeni.

"Nancy amkia wageni. Yaani mwanangu pengine kutokana na kukaa ndani muda mrefu hapendi kuongea hata kujichanganya na watoto wenzake. Akikaa hapo kwenye tv, utapita muda mrefu bila kunyanyuka, labda kwa sababu ya matatizo yake.

"Ili kulinda utu wa mwanangu inanipasa niwe na shilingi 2,000 au 3,000 kwa siku, ili ninunue pampers za saizi yake, ana miaka nane, nisipofanya hivyo nimfungie ndani asitoke wala kwenda shule," Mama Nancy anatamka.

"Mwanangu ana miaka nane na muda mwingi ina nibidi nishinde naye mimi mwenyewe, huwezi kumuachia na mtu, utamkwaza. Anahitaji huduma za karibu mara kwa mara. Anavaa pampasi kila siku, inanipasa niwe na pesa kila siku, baba yake aliondoka akaniachia ulezi," anasema mama huyo.

> **"Kwa sababu kwa hali yake utamuachia nani, itakuwa lawama! Nikitoka usiku kwenda katika biashara, namuacha peke yake anaangalia televisheni hadi ninaporudi saa nne usiku.**

"Inaniwia vigumu kwa sababu shughuli yangu ni ujasiriamali mdogo, nauza karanga mbichi na za kukaanga, pamoja na sigara, ikifika usiku hapo kituoni Rosana. Biashara ya saa nne lakini nagawanya moyo. Ukiwa kwenye biashara wazo moja lipo kwenye biashara na lingine nawaza nyumbani nilikomuacha mtoto.

"Kwa sababu kwa hali yake utamuachia nani, itakuwa lawama! Nikitoka usiku kwenda katika biashara, namuacha peke yake anaangalia televisheni hadi ninaporudi saa nne usiku. Mara nyingine namkuta yupo macho au kalala hapo hapo kwenye kochi," mama huyo anaeleza

Mama Nancy ni kati ya walezi wengi wenye simulizi tofauti kuhusu watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi. Nancy ana kichwa kikubwa na mgongo wazi tatizo lililogunduliwa siku chache baada ya kuzaliwa.

"Nilipojifungua mtoto wangu wa kiume nilipokuwa Zanzibar nikiishi na mume wangu, alifurahi sana. Siku chache kichwa kilianza kuongezeka ukubwa. Mume akanitoroka," anasimulia Mama Goodluck.

"Nimemlea mtoto huyu mwenyewe kabla hajaanza hata shule ya msingi, sasa yupo kidato cha tatu, mama yake aliniachia mtoto," anasema baba Alfeo.

Katika mazungumzo maalum na Nipashe, Mama Nancy anaeleza hayo kwenye kambi ya siku tatu iliyoandaliwa na Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi (ASBAHT), viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Chama hicho kinasema utafiti wao, umebaini wazazi wa watoto hao na hasa kinamama, mahusiano na wazazi wenza yamekatizwa kutokana na ujio wa mtoto aliyezaliwa hivyo, malezi duni na kukosa mahitaji.

Mama Nancy, anasema ni kawaida jamii kuwaita majina tofauti yanayowafanya wajihisi uzazi wao umeikosea jamii. Pia, anakiri matibabu ya mtoto huyo ni ghali, akisema kifaa cha mrija unaosaidia kunyonya maji kichwani (shunt) hakimo kwenye orodha ya vifaa tiba vinavyotolewa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), na kwamba hupata msaada kutoka shirika la Child Help International.

Oliva Mbimbi, akiwa mjasiriamali wa kuuza bidhaa kama sabuni anakoishi, kutokana na uhalisia wa kushindwa kumuacha mwanawe pekee au kumuachia mtu kutokana na tatizo alilo nalo.

Oliva, mzazi wa mtoto Goodluck Hassan (6), anasema alipojifungua mtoto alikuwa wa kawaida na mwenye afya na baada ya muda wa wiki chache akaanza kuongezeka ukubwa.

"Alianza kubadilika na ndipo nikarudi hospitali. Baba yake alinitoroka baada ya kumuona kichwa kinaongezeka. Mwanangu alifanyiwa upasuaji baada ya miaka mitatu akawekewa 'shunt' sasa anaendelea vizuri," anasema Oliva.

Mama huyo anaendelea; "Changamoto ni lishe, elimu ya saikolojia kwa sababu muda mwingi unawaza, wazazi wenye watoto hawa wengi tuna mtoto mmoja yaani ukimzaa mtoto wa aina hii, ni kama uzazi wa mpango, unaogopa hata kurudia kuzaa tena."

"Tunaitwa majina mengi; wamama wenye watoto matahira, bichwa maji, walemavu, yaani jamii inatutafsiri tofauti na wengine ukiongozana na mtoto barabarani unageuka 'topic' (mada), watu wanakushangaa hadi unaona aibu," anaeleza.

Anafafanua kuwa mtoto wake anahitaji huduma za afya kila mara, akaamua kumkatia 'Bima Toto' inayotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na alifanikiwa kumpeleka mtoto wake CCBRT kwa matibabu.

"Kuna gharama, kwa siku inatakiwa ale milo mitatu iliyokamilika. Changamoto aliyonayo sana ni hana kumbukumbu hata akiwa na njaa hasemi, akishiba hasemi, atakaa tu, anakuangalia.

"Chakula umpimie, usipopima anaweza kula chakula kingi hadi cha watu wawili akavimbiwa. Inabidi kama mama nihesabu saa ambazo atahitaji mlo ukimuachia mtu hawezi kufuata utaratibu huu, atashinda na njaa, hana hisia za njaa, anaweza akashinda toka asubuhi hadi usiku bila kula," anasimulia Oliva, mzazi wa Goodluck.

Anaeleza, kwa sasa mwanawe yuko katika shule ya awali, binafsi akitaka mtoto wake akajichanganye na wenzake, ingawa hafahamu alichofundishwa na akirudi nyumbani anapomuuliza alichojifunza, anakosa majibu.

"Ada ninamlipia sh. 40,000 kila mwezi, nilikuwa nina shughuli ya mama lishe ila muda mwingi nashindwa kufanya shughuli zangu, labda nimuachie dada yangu akae nae."

**HOSPITALINI MOI**

Daktari bingwa kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Laurent Mchome, anasema taasisi hiyo inapokea watoto 700 hadi 1,200

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Yanayowasibu walezi wa watoto vichwa vikubwa na mgongo wazi

INATOKA UK.12

kwa mwaka wenye tatizo la vichwa vikubwa na mgongo wazi, chanzo kikuu ikiwa lishe duni kwa wajawazito.

"Kati ya watoto 100 wanaozaliwa, watoto wawili hadi watatu wana uwezekano wa kuzaliwa na tatizo la mgongo wazi au kichwa maji. Tatizo linatokana pengine kabla ya kuzaliwa yaani wakiwa tumboni au baada ya kuzaliwa," anasema Dk. Mchome.

"Tatizo huanzia tumboni mwa mama zao kabla ya kuzaliwa katika kipindi cha miezi mitatu ya ujauzito. Iwapo mama mjamzito atakosa madini ya chuma na lishe bora," anasema Dk. Mchome.

MOI inasema Tanzania ina watoto 4,800 wanaozaliwa kila mwaka, kati yao 700 hadi 1,200 hupokelewa. Anataja, kundi lingine ni ambao baada ya kuzaliwa walipata majeraha kwenye ubongo na damu kuvilia ndani.

"Awali ilikuwa tunapokea watoto wenye tatizo hili kutoka Morogoro maeneo ya Ifakara, Mahenge au Kanda ya kati. Haikufahamika ni kwa nini, lakini hivi sasa wagonjwa hao wanatoka mikoa mbalimbali nchini," anaeleza bingwa huyo.

Bingwa huyo anataja dalili zao ni kuwa na nundu mgongoni na kupata shida ya haja ndogo, hata kushindwa kutembea na kwamba wakipata tiba mapema, hupona.



Olivia Mbimbi akiwa na mwanaye Goodluck, kwenye maadhimisho Siku ya Watoto Wenye Vichwa Vikibwa na Mgongo wazi, yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

### TIBA YA MRIJA

Daktari Bingwa wa Fahamu na Ubongo MOI, Dk. Hamis Shaban, anasema asilimia 40 ya watoto wanaopatiwa matibabu ya kuwekewa mrija wanapata tatizo, hivyo wataalamu wakaamua kuja na tiba mpya ya kutumia matundu.

"Shunt hutumika kunyonya maji kwenye mishipa iliyoko kichwani na kuyaelekeza tumboni, ili yaingizwe kwenye mzunguko wa kawaida," anasema bingwa huyo.

Bingwa huyo anabainisha njia inayopendekezwa kwa sasa na wataalamu ni kutumia kifaa 'Endoscopic Third Ventriculostomy (ETV)' ambacho mtoto mwenye kichwa kikubwa anawekewa kichwani ili kuua sehemu inayozalisha maji, kuzibua mishipa kupitisha maji kwenda katika maeneo (vyumba vinne) vya kichwa.

"Mrija (shunt) unaweza kuziba kutokana na chembechembe zilizoko katika maji yanayotoka kichwani, kuachana kwenye maungio au kupwaya kichwani na kuleta michubuko na kuhatarisha ubongo, anasema.

Anafafanua wakati kuna mazingira yanayomhatarisha mtoto kufanyiwa upasuaji zaidi ya mara mbili, ETV inakuwa mbadala ambao akishawekewa mfumo, inafuta haja ya upasuaji tena.

"Siyo kwamba, uwekaji wa mrija umeachwa, bado tunaendelea nao MOI, ni uamuzi wa mzazi au mlezi kuona ni njia ipi atumie kuondoa tatizo hili, lakini ninapendekeza ETV," anasema bingwa huyo.

### HUDUMA YA CIC

Ignace Mvungi, Ofisa Muuguzi kutoka MOI na mtaalamu wa kuwawekea kifaa kiitwacho CIC, mahsusi kuwakinga na maradhi ikiwamo UTI, pia kulinda utu wao kwa sharti la kuwa karibu na mtoto, huwa kila baada ya saa kadhaa, anahitaji kupelekwa haja.

Anafafanua:"Kifaa hiki huwekewa hata mtu mzima aliyepata ajali 'spinal cord' au baadhi ya pingili za uti wa mgongo zimepata shida na kutopata hisia za mkojo na haja kubwa."

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, CIC mvaaji hajijui hata kama amevaa, ingawa tatizo lililopo havipatikani nchini, vinatolewa kupitia shirika la Child Help.

> Watoto wenye tatizo hilo baadhi hunyanyapaliwa, huku wengine wakifukuzwa shule wakikoseshwa haki ya elimu.

### WADAU WASAIDIZI

Janeth Manoni, Mratibu wa Shirika la Child Help International Kanda ya Afrika, anasema wamekuwa wakitoa vifaa tiba na mwaka 2020 wametoa mirija 1,625 yenye thamani zaidi ya Sh.Milioni 100.

Pia, Hidaya Alawi, Mratibu wa Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi (ASBAHT), anasema watoto wenye tatizo hilo baadhi hunyanyapaliwa, huku wengine wakifukuzwa shule wakikoseshwa haki ya elimu.

"Mfumo wa maisha, lishe duni, maandalizi duni ya wenza watarajiao kupata watoto, mila na dhana potofu vinasababisha tatizo kuendelea miongoni mwa jamii huku wenza wakitelekezeana watoto hao wakidai ni laana," anasema Hidaya, akitaja asilimia 78 (robo tatu) ya kinamama wanaojifungua watoto wenye tatizo hilo, wanakimbiwa na waume.

Anasema vikwazo vingine ni kukosa tiba kupitia bima ya afya, gharama za vipimo kuwa kubwa, wazazi kupata msongo wa mawazo kutokana na kukosa huduma za matibabu kwa watoto wao na kwamba asilimia 99 ya matibabu yao huwategemea wahisani.

Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dk. Milka Mathania, anaiambia Nipashe kuwa tatizo linaongezeka nchini, Dar es Salaam ikiwamo kwa wenye idadi kubwa.

## ...Yajue yanayowakaribishia wengi maradhi figo

**Na Mwandishi Wetu**

ULAJI nyama kwa wingi, uvutaji sigara, pia pombe kunatajwa ni miongoni mwa vinavyochangia kupata magonjwa yasiyo ya lazima, ikiwamo kwenye figo.

Ugonjwa figo unatajwa kuwatesa wengi hata pale mgonjwa anapoanza huduma za kusafisha figo, anaangukia shida nyingi ikiwamo ya gharama kubwa kila anaposafisha figo.

Hivi karibuni, imeelezwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, kumefanikiwa kuwapandikiza figo wagonjwa 26 kuanzia Machi 22, 2018 kutoka mikoa mbalimbali nchini na wote wanaendelea vizuri kiafya.

Mkuu wa Magonjwa ya Figo hospitalini hapo, Dk. Anthony Gyunda, anafafanua: "Uharibifu wa Figo unasababishwa na taka sumu pamoja na magonjwa yote yanayoathiri mwili kama kisukari, shinikizo la damu pamoja na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza."

"Kuna hatua tano za matibabu. Ukigundulika na ugonjwa wa figo ikiwapo hatua ya haraka ambayo ni uchujaji wa damu na hatua ya mwisho ni upandikizaji wa figo," anaeleza Dk. Gyunda

Pia, anatumia wasaa huo kutoa ushauri kwa wananchi kuepuka ulaji nyama kwa wingi, utumiaji sukari, mafuta ya kula na unywaji pombe kulikopitiliza, ili kuepuka magonjwa yasiyokuwa ya lazima, ikiwamo hayo ya figo.

"Epukeni matumizi holela ya dawa, nendeni mkapate vipimo na ushauri wa wataalamu kwa kuwa matumizi ya dawa kiholela sio mazuri kiafya na hii huchangia kuua mfumo wa figo," anasema Dk. Gyunda

Kingine anachoshauri tabibu huyo ni haja ya wananchi kupata vipimo kila mara, walau mara mbili kwa mwaka, ili kujua undani wa afya zao na kuepuka gharama za matibabu.

Anasema, katika hospitali wanapokea wagonjwa mbalimbali kutoka mikoa jirani, akitaja baadhi kuwa ni Iringa, Singida na Manyara.

Pia, anatumia fursa hiyo kuishukuru serikali kupitia Wizara ya Afya, kwa kuwawezesha kupata watumishi wenye weledi, ikiambatana na vifaa tiba sahihi.

Mmoja wa wagonjwa wa figo, ambaye ni ana umri miaka 17, anaeleza anapata matibabu ya uchujaji wa damu katika hospitali hiyo na anaendelea vizuri.

Mtaalamu wa Magonjwa ya Uti wa Mgongo, Dk. Waziri Jimmy, anasema sio lazima kila tatizo kufanyiwa upasuaji, bali magonjwa mengine yanapaswa kuisha kupitia dawa.

"Ili kujua tatizo mapema, lazima kupata vipimo kwa kuwaona Wataalamu kabla ugonjwa haujazidi hadi kupelekea kufanyiwa upasuaji," anasema Dk. Jimmy

Kitaaluma katika mustakabali wa afya, magonjwa yasiyoambukizwa huwa mara nyingi hayana dalili, hivyo ni muhimu kwa mtu kujua afya yake kabla ya tatizo kujitokeza.

MAZINGIRA

MSITU MPYA MABWEPANDE....

# TAWA ilivyojikita kubadili Pori la Akiba Pande lisibaki kisiwa

• Serikali ya mtaa, shule zahamasika 'kisawasawa'



Baadhi ya viongozi wa Serikali ya Mtaa wa Mabwepande, walimu, wanafunzi na watumishi wa Pori la Akiba Pande wakiwa wameshika miti ya matunda na vivuli kwa ajili ya kupanda, ili kutunza mazingira. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

**Na Christina Haule**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imeanzisha mradi wa maboresho ya kupanda miti katika eneo lote linalouzunguka Msitu wa Hifadhi wa Pande, uliopo ndani ya wilaya za Kinondoni na Ubungo Jijini Dar es Salaam.

Kimsingi, msitu wa Pande ni kati ya mapori 20 ya akiba yaliyopitishwa kisheria kusimamiwa na TAWA. Meneja wake, Honest Buletta anasema tukio la upandaji miti kwenye eneo la Shule ya Msingi Mabwepande, ulilenga kuondoa hali ya msitu huo kuonekana 'kisiwa' kinachozungukwa na makazi, sasa liwe kwa upana unaohifadhi mazingira.

Kwa mujibu wa Buletta, jumla ya miti 170 ilipandwa shuleni hapo kati ya 600 inayotarajiwa kupandwa katika kipindi cha mwezi mmoja kwenye eneo hilo kuzunguka pori , huku dira iliyoko ni kupanda miti 250,000 katika mwaka mmoja hadi miwili ijayo,

Anasema, ni namna inayolenga kupafanya paonekane msitu mnene kutoka makazi ya watu pekee, ikiwa ni kampeni endelevu ya upandaji miti inayofanyika kwa kushirikiana na wananchi katika maeneo hayo na wanajumuiya na taasisi kama vile shule, hospitali, taasisi za kiserikali ili kulinda na kuhifadhi mazingira.

**WADAU WASHIRIKI**

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mabwepande, Mwalimu Mangwala, anaishukuru TAWA kupitia pori la Akiba la Pande kwa kuonyesha ushirikiano mzuri katika mambo mengi ya kuinua maendeleo ya mtaa huo, ikiwamo kuhamasisha upandaji miti na katika kupokea wageni maalumu wanaokuja kwenye kata hiyo.

> **Mamlaka ya TAWA-Pande, imekuwa ikitoa elimu kwa wanafunzi kuhusu utunzaji mazingira na wanafunzi wenyewe wanafanya utalii wa ndani kujua vitu vilivyomo.**



Meneja wa Pori la Akiba Pande, Honest Buletta akipanda mti katika Shule ya Msingi Mabwepande, ikiwa ni moja ya uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti 250,000 katika maeneo yanayopazunguka.

Hivyo, anaiomba jamii kutikia wito wa upandaji miti katika maeneo mbalimbali ili kufikia lengo la TAWA na hata kuboresha mazingira yao. Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mabwepande, Victor Kamoli, anasema wameamua kuanzisha klabu ya mazingira ili kujiimarisha kimazingira, pia kuwajengea uwezo watoto kujua umuhimu wa utunzaji mazingira.

Anasema elimu ya mazingira wanayopewa wanafunzi shuleni, inawasaidia watoto hata majumbani kudhibiti uharibifu wa mazingira kwenye ngazi ya familia zao, huku wakijiimarisha katika upandaji miti.

Mwalimu Kamoli anaishukuru TAWA kupitia pori la Akiba Pande kwa kuwasimamia, hata tayari wameshapanda miti 170, katika mgawanyiko wa miti ya matunda ya kopo 60 na 110 ni ya vivuli.

Anasema Mamlaka ya TAWA-Pande, imekuwa ikitoa elimu kwa wanafunzi kuhusu utunzaji mazingira na wanafunzi wenyewe wanafanya utalii wa ndani kujua vitu vilivyomo.

Mwalimu Kamili anadokeza kuwa, wapo wanaokaa Mabwepande, lakini hawajui kilichomo ndani ya pori wanalolizunguka wakilitunza, hivyo anasema watoto hao kupitia elimu wanayopata hupeleka elimu hiyo kwa wazazi wao kuhusu umuhimu huo nao wakaelimika.

Anaeleza jinsi wanavyomudu kuitunza miti waliyokabidhiwa na kutorudisha nyuma juhudi za upandaji miti katika msitu wa Pande. Anatambulisha umri wa klabu ya mazingira kuwa ipo tangu mwaka 1978 shule ilipoanzishwa, lengo lake ni kuimarisha na kulinda mazingira yanayoizunguka.

Pia, anataja kuwapo ajenda ya kuwaweka vizuri wanafunzi katika utunzaji mazingira wawapo majumbani akiwa katika imani ya kitaaluma "utunzaji wa mazingira ni mzuri, kwa sababu na yenyewe yanawatunza."

Katibu wa Bright Vision Tanzania, shirika linalojishughulisha na masuala ya mazingira nchini, Oscar Samson, anahimza kushirikiana na mradi wa Pori la Akiba Pande chini ya TAWA, kupitia miradi endelevu ya utunzaji mazingira, na kwamba wamefanikiwa kutafuta miti na kuanza kupanda katika maeneo yanayozunguka pori hilo.

Anasema mradi huo unatoa elimu ya mazingira na kusaidia maeneo yenye changamoto za mazingira, Samson akisema ni kilio cha dunia kinapopoteza uasili wake kutokana na ukataji wa miti. Anatoa angalizo kwa wananchi kutumia elimu sahihi wanazopewa kuacha kukata miti na uchomaji mkaa ovyo na mengine yanayoharibu mazingira.

Pia, anaiasa jamii akiitaka ibadilike kutokana na majanga ya mazingira wanayoyaona ikiwamo ukame na mabadiliko ya tabianchi, sasa wamejipanga kuelimisha wanafunzi wakawe mabalozi wakubwa na kuelimisha jamii inayowazunguka kuhusu utunzaji mazingira, ikiwajumuisha walimu na wakazi wengineo.

Mwenyekiti wa Klabu ya Mazingira Shule ya Msingi Mabwepande, Caroline Joseph, mwanafunzi wa darasa la sita, anawaomba wadau wa mazingira, ikiwamo serikali kuwasaidia kujenga uzio utakaowasaidia kuendeleza juhudi za utunzaji mazingira shuleni hapo.

Anasema kuna watu wanaokatiza katika eneo la shule hiyo wanafunzi wakiwa madarasani, wanakanyaga miti na maua au kuangusha uchafu kwenye eneo la shule na kufanya mwingiliano usio wa lazima, jambo linaloweza kudhibitiwa kupitia uzio.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kibesa, wilayani Ubungo, Dar es Salaam, Nestory Masunga anasema katika Pori la Akiba Pande, TAWA imekuwa msaada kwao katika utoaji elimu kwa wanafunzi katika masuala ya utunzaji mazingira, ambayo ina jumla ya miti 130 ikiwamo ya kivuli na matunda imepandwa.

Rai yake ni kwa TAWA kuendeleza juhudi, kwani tayari imeshawapa hamasa na wameona umuhimu wa mazingira kwa tafsiri pana.



# Serikali yawatega watendaji h'shauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema haitamvumilia mtendaji yeyote wa Halmashauri atakayekwenda kinyume cha malengo ya serikali kwenye usimamizi wa miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Switbert Mkama, alitoa kauli hiyo jijini hapa kwenye kikao kazi kilichowakutanisha wakurugenzi wa halmashauri za mkoa wa Dodoma lengo likiwa ni kuwakumbusha majukumu yao waliyopewa katika kusimamia na kutoa matokeo chanya yaliyokusudiwa na Serikali katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Alisema hajaridhishwa na utendaji kazi wa baadhi ya wakurugenzi na wakuu wa idara kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kisheria na kidhamu na kusababisha kushindwa kusimamia miradi kwa weledi.

"Mnatakiwa kusimamia miradi kwa weledi, mtambue kuwa lengo la miradi hiyo ni kuwawezesha wananchi kupata huduma bora, simamieni miradi hiyo kwa makini msilete mazoea kwenye miradi, wengi wenu mnasimamia bila ya kufuata utaratibu ,"alisema.

"Serikali haitavumulia hili niwaambie Sheria, Kanuni na Taratibu za kinidhamu zitachukuliwa kwa kiongozi na mtumishi yoyote atakayefanya kazi kwa mazoea na kwenda kinyume cha sheria na taratibu za Serikali katika utekelezaji wa miradi inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa," alisema.

Alibainisha baadhi ya Halmashuri hazifuati utaratibu katika kufanya ununuzi, kubadilisha matumizi ya fedha na utoaji wa mikopo ya Serikali kwenye vikundi vya wakinamama, vijana na watu wenye ulemavu.

"Nitoe onyo watumishi watakaobainika kwenda kinyume na utaratibu hatua kali za kisheria zitachukuliwa,"alisema.

Kuhusu kushuka kwa ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya halmashauri nchini, aliwataka kutoharibu mashine za ukusanyaji wa mapato.

Kwa upande mwingine, Naibu Katibu Mkuu Ofisi hiyo anayeshughulikia Afya, Dk. Grace Magembe, alisisitiza suala la utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kukamilisha miradi haraka ili kuwapunguzia wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za kijamii.

"Niseme tu kama huwezi kuhudumia wananchi maana yake hutoshi kukaa katika kiti ulichokalia kwa sababu serikali imetuamini ili tusimamie miradi na tuwahudumie wananchi katika utoaji wa huduma bora" alisema.

# Mkenda awaombea fedha wanaosoma nje

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema ipo haja kwa serikali kutenga fedha kwa ajili ya kupeleka katika vyuo vya nje wanafunzi bora wa masomo ya sayansi ili kujifunza na kuwa wabobezi katika masuala ya nguvu za Atomiki.

Prof. Mkenda alibainisha hayo juzi katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa maabara na ofisi za Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kanda ya kati katika eneo la Kikombo jijini hapa.

"Kama tunataka kufanikiwa lazima kuwekeza katika elimu, watu wanaweza kuona kuwa kuwekeza kwenye jengo ndiko upo umuhimu kwa vile linaonekana lakini kwa wakati wa sasa taaluma ya masuala ya nguvu za Atomiki ni muhimu sana."

"Hivyo sasa ni lazima tuanze kupanga bajeti kwa ajili ya kupeleka vijana wetu ambao wamefanya vizuri katika masomo yanayoendana na nguvu za Atomiki ili wakirudi watusaidie," alisema na kuongeza:

"Leo hii watu wanasema nchi kama Singapore ambazo zilikuwa sawa na Tanzania miaka ya nyuma zimeendelea kutokana na kuwekeza katika elimu."

Aidha, alisema utaalamu katika masuala ya nguvu za atomiki ni muhimu sana kwa sasa ambapo Tanzania imejiwekea azma yake ya kufikia uchumi wa viwanda.

"Desemba mwaka huu tutakuwa na mkutano mkubwa na wahadhiri wa vyuo kutoka maeneo mbalimbali duniani ili kujadili ni namna gani tunaweza kupata fursa za vyuo vya masuala ya nguvu za atomiki ili kupeleka vijana wetu wakapikwe huko,"alisisitiza Prof. Mkenda.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC), Prof. Lazaro Busagala, alisema ujenzi huo unahusisha maabara pamoja na ofisi ambapo utagharimu Sh. bilioni 3.8.

"Mheshimiwa Waziri, kwanza tukushukuru kwa wizara yako kutupatia hadi sasa zaidi ya asilimia 90 ya fedha zilizotengwa kwenye bajeti yetu, ujenzi huu ni wa mwaka mmoja na tulitiliana saini na mkandarasi Mei, mwaka jana na mpaka sasa hatudaiwi ila tunadai kazi,"alisema.

Hata hivyo, alisema kukamilika kwa ujenzi wa ofisi hiyo na maabara kutasaidia kusogeza huduma ya masuala ya kudhibiti mionzi jirani na wananchi.

Kadhalika, alisema moja ya majukumu ya Tume hiyo ni kudhibiti uingizaji wa bidhaa zenye mionzi katika maeneo ya mipaka ya nchi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya jamii, Abdallah Chikota, alisema Bunge litaendelea kutoa ushirikiano kwa tume hiyo ili kutekeleza majukumu yake.

"Sisi wabunge tumeridhishwa na ujenzi huu wa ofisi pamoja na maabara na hatutakuwa kikwazo kwa juhudi zenu na kazi mnazozifanya katika kusogeza jirani na wananchi huduma hizi na masula ya nguvu za atomiki," alisema Chikota.



Naibu Waziri Ofisi Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge kwenye vikao vya Bunge vinavyoendelea jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma sasa kuwekewa anuani makazi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MITAA 222 iliyopo ndani ya kata 41 za Halmashauri ya Jiji la Dodoma inatarajiwa kuwekewa anuani za makazi ili kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali.

Mratibu wa mfumo wa uwekaji anuani za makazi jiji hapa, Joseph Nkuba, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Nkuba alisema kuwa mitaa hiyo itakayowekewa itaongeza ufanisi kwenye mitaa mbalimbali katika kufikisha bidhaa na kuzuia upotevu na wananchi kurahisishiwa kutambua makazi yao.

Alitaja faida zingine kwenye anuani hizo kuwa ni kurahisisha huduma za ulinzi na usalama, kuongeza ufanisi katika usimamizi wa makazi ya watu na kutambua mali na upatikanaji wa takwimu mbalimbali.

Zingine ni kuongeza tija na ufanisi katika huduma za uokoaji na maafa, kuwezesha ukusanyaji wa kodi mbalimbali kwa urahisi na kwa wakati ikiwa na pamoja na kupambana na uhalifu katika kupata taarifa za uhamiaji na shughuli za utalii.

"Uwekaji wa anwani za makazi ulianza Desemba 13,2021 kwa ajili ya kutambua mipaka ya mitaa 153 na hadi sasa iliyobaki ni mitaa 69 na itakamilishwa ifikapo Mei, 22 mwaka huu."alisema.

Vilevile alisema kuwa jiji linatarajia kuajiri vijana 100 wenye sifa ikiwemo ya elimu ya kidato cha nne, wataalamu wa kutumia kompyuta na wale wenye uwezo wa usomaji wa ramani ambapo watafanya kazi hiyo kwa siku 45.

Mratibu huyo alitoa tahadhari kwa wananchi kuihusisha shughuli hiyo na upimaji wa viwanja, badala yake wawe na ushirikiano kwa serikali ili kukamilika kwa wakati.





# Vijana wanufaika na mitaji uboreshaji mazao biashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA wenye mawazo bunifu ya biashara ya mazao ya mboga na matunda wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameanza kunufaika na programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT kwa kupatiwa mitaji.

Programu hiyo ambayo inaendeshwa kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) na serikali ya Tanzania, inatekelezwa katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na Zanzibar na inalenga kuboresha miundombinu ya masoko na barabara.

Shirika lisilo la kiserikali la RIKOLTO ambalo ni miongoni mwa watekelezaji wa programu hiyo, linatarajia kutumia zaidi ya Sh. milioni 700 kuwanufaisha vijana 400 wenye mawazo bunifu ya biashara na ujasiriamali.

Mratibu wa RIKOLTO, Shukuru Tweve, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa kupokea na kushindanisha mawazo ya kibiashara ya vijana 26 kutoka mikoa minne ya ukanda huo. Alisema zaidi ya vijana 100 walishiriki kwenye shindano hilo.

Alisema katika awamu ya kwanza, vijana kutoka Mbeya, Njombe, Songwe na Katavi walishiriki kushindanisha mawazo yao na kati yao, 18 walishinda na kupatiwa mitaji ya kuendeleza biashara zao.

"Vijana hawa 18 wameelezea mawazo yao na kuonyesha kwa vitendo namna ya utekelezaji, lakini jambo hili ni endelevu na fedha zilizotengwa ni nyingi sana, kwa hiyo tunaamini mawazo haya yatasaidia vijana hawa kujiajiri," alisema Tweve.

Mratibu wa AGRI-CONNECT wa Mkoa wa Katavi, Frank Kaminyoge, alisema fedha walizopewa vijana ambao mawazo yao yalishinda ni kuendeleza kilimo cha mboga na matunda katika maeneo yao.

Pia alisema fedha hizo zitatumika kwenye uendelezaji wa biashara za mboga na matunda pamoja na kuendeleza viwanda vya kuchakata mazao hayo kila mmoja kulingana na alivyowasilisha.

Lengo la mradi huo, alisema ni kuhakikisha wakulima wanauza mazao yao baada ya kuyaongeza thamani badala ya kuendelea kuuza mazao ghafi ambayo alisema tija ya soko lake ni ndogo kuliko wakiuza mazao ambayo yamechakatwa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, aliwataka vijana wanaopatiwa mitaji hiyo kuhakikisha wanaitumia kwa malengo yanayokusudiwa na wafadhili.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa hiyo ya AGRI-CONNECT kufanya biashara zao na shughuli za kilimo kwa kuwa ni sehemu ya ajira zinazoajiri watu wengi.

"Hakikisheni mnatumia vizuri hii fursa. Hizi fedha zinazoletwa na wafadhili hakikisheni mnazitumia kwa ajili ya biashara ya mazao ya mboga na matunda kama inavyotakiwa," alisema Dk. Chuachua.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, akikagua bidhaa za baadhi ya vijana walioshiriki kwenye shindano la mawazo bunifu ya biashara na ujasiriamali katika mazao ya mboga na matunda lililoendeshwa juzi na Shirika la RIKOLTO chini ya ufadhili wa programu ya AGRI-CONNECT. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waliovuliwa uongozi wadai bado viongozi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Wilaya ya Mbeya Mjini waliovuliwa nafasi zao na Kamati Tendaji ya chama hicho Kanda ya Nyasa, wameendelea kutunisha misuli wakidai kuwa bado ni viongozi.

Akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo la Mbeya Mjini, Mwenyekiti wa viongozi hao waliotumbuliwa, John Mwambigija, alisema viongozi wa chama hicho wa Kanda waliotangaza kuvunja uongozi wao ni sawa na waasi.

Mwambigija alisema Kamati Tendaji ya Kanda ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mchungaji Peter Msigwa ni sawa na waasi ambao wanataka kupindua uongozi wake isivyo halali.

Alisema wao ni viongozi ambao walichaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya CHADEMA ya mwaka 2006 pamoja na maboresho yake ya Mwaka 2019, hivyo hawako tayari kuondolewa madarakani bila kufuata taratibu za kisheria.

Kiongozi huyo aliwataka wanachama na viongozi wa chama hicho ngazi ya kata na wilaya kuendelea kuwaamini ili wafanikishe malengo yao ikiwemo ujenzi wa Ofisi ya Chama ngazi ya jimbo huku akisema wanapigwa vita kwa sababu ya maendeleo wanayofanya.

"Wenye mamlaka ya kuuondoa uongozi wa chama uliochaguliwa ni Mkutano Mkuu wa Chama na si vinginevyo. Kwa hiyo naomba puuzeni uamuzi unaofanywa wa kutaka kutuondoa madarakani," alisema Mwambigija.

Alisema Mchungaji Msigwa na wenzake ndio waliovunja katiba ya chama hicho kwa kuchukua mambo ya chama na kuyapeleka kwenye vyombo vya habari wakati katiba inazuia kufanya hivyo.

Hivi karibuni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Mch. Msingwa alitangaza kuwa Kamati Tendaji ya Kanda hiyo imewavua uongozi viongozi wote wa Kamati Tendaji ya Chama hicho Wilaya ya Mbeya Mjini ikiongozwa na mwenyekiti wake, John Mwambigija.

# Bil. 1.4/- kujenga daraja lililoua watu watano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mto Tembela ambalo lilivunjika mwaka 2019 na kusababisha vifo vya watu watano.

Licha ya kusababisha maafa hayo, daraja hilo pia lilikata mawasiliano ya kata tatu za Jiji la Mbeya kwa zaidi ya miaka miwili.

Daraja hilo linalounganisha kata za Mwakibete, Tembela na Mwasanga pamoja na baadhi ya kata za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na baadhi ya wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakikosa huduma muhimu kwa kipindi hicho.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alifanya ziara katika eneo hilo juzi na kuwapa matumaini wananchi kwamba serikali imeshatenga fedha hizo kwa ajili ya kurejesha mawasiliano.

Alisema serikali imetenga fedha hizo na tayari zimeshaingizwa kwenye akaunti ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Bashungwa alisema serikali ilitenga fedha hizo baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan.

Alimuagiza Meneja wa TARURA Mkoa wa Mbeya kuhakikisha daraja hilo linaanza kujengwa kabla ya Machi Mosi, mwaka huu, ili mawasiliano yarejee haraka na wananchi waendelee kulitumia kwa ajili ya shughuli zao za kijamii na kiuchumi.

"Nataka inapofika Machi Mosi Meneja unitumie video na picha zikionyesha mkandarasi akiwa hapa anaendelea kujenga daraja hili. Fedha tayari unazo, hivyo nitakuwa nafuatilia ili kuhakikisha mawasiliano yanakamilika," alisema Bashungwa.

Alisema kutokana na umuhimu wa barabara hiyo kwa halmashauri zote mbili, serikali itaangalia namna ya kuiweka kwenye mipango yake ili ijengwe kwa kiwango kinachoruhusu kupitika mwaka mzima.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa kata ya Tembela, Diwani wa Kata hiyo, Frank Mwasyoke, aliishukuru serikali kwa kuwajengea daraja hilo kwa maelezo kuwa uchumi wa wananchi ulikuwa umeanza kudumaa.

Mwasyoke alisema wananchi wa eneo hilo hasa katika kata za Mwasanga na Tembela, shughuli zao kuu ni kilimo ambacho soko lake ni maeneo ya Mbeya mjini lakini daraja hilo lilikuwa linawakwamisha.

Alisema ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika, wananchi wa kata hizo waliamua kuungana na kujenga daraja la muda pamoja na kupanua barabara kwa kuilima kwa jembe la mkono.

Aliiomba serikali iwasaidie kujenga barabara hiyo vizuri kwa maelezo kuwa kwenye daraja hilo kuna mlima mkali katika pande zote mbili hali ambayo huwa inaleta shida yanapopita magari yenye mizigo.





# SMZ kuboresha majengo ya mahakama

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakusudia kufanya maboresho makubwa katika ujenzi wa Mahakama za Unguja na Pemba na kwa kuanzia, kazi hiyo itafanywa katika Mahakama za Mkokotoni na Konde Mkoa wa Kaskazini Pemba. Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akijibu swali la nyongeza la Mwakilishi wa Wete, Harusi Said Suleiman

Harusi alitaka kujua mipango ya serikali ya kuimarisha majengo ya mahakama na kutaka kujua lini jengo la Mahakama ya Wete litafanyiwa ukarabati.

Waziri Suleiman alisema amefanya ziara ya mikoa mitano ya Zanzibar kwa ajili ya kukagua majengo ya mahakama ikiwa ni sehemu ya mikakati ya serikali kuimarisha majengo hayo ili kutoa huduma za kisheria na haki kwa wananchi.

Alisema kwa kuanza ukarabati huo, wataanza na jengo la Mahakama ya Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa sababu iko katika hali mbaya na haikidhi vigezo katika kutoa huduma za kisheria na hukumu kwa wananchi.

"Mimi binafsi nilitembelea jengo la Mahakama ya Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja na kujionea uchakavu wake ambao unatishia maisha ya wafanyakazi, hivyo tutalifanyia matengenezo makubwa hivi karibuni," alisema.

Pia alisema serikali inakusudia kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la Mahakama huko Konde Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kuwawezesha wananchi kupata huduma za kimahakama.

Alisema ni kweli jengo hilo limepitwa na wakati likiwa halina nafasi ya kutosha ya kuwawezesha wananchi kusikiliza mashauri yao kikamilifu.

"Tutafanya ukarabati mkubwa jengo la Mahakama ya Konde pamoja na jengo la Mahakama ya Wete kwa sababu majengo haya yamejengwa zamani sana kabla ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964," alisema.

Waziri alisema juhudi za kuimarisha majengo ya mahakama kubwa bora na ya kisasa zimezaa matunda kutokana na serikali kujenga jengo la Mahakama Kuu, Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

## Barabara bora kujengwa kwenda hoteli za kitalii

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, amesema atahakikisha barabara za ndani zinazokwenda katika miradi ya hoteli za kitalii zinajengwa ili kurahisisha usafiri.

Aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Nungwi, Abdallah Abbas Wadi, aliyetaka kujua lini serikali itazifanyia ukarabati barabara zinazokwenda katika hoteli za kitalii zilizoko Nungwi.

Waziri huyo alisema ni kweli katika kijiji cha Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuna hoteli nyingi za kitalii ambazo zimekuwa zikisaidia kuingiza mapato na kutoa ajira kwa wananchi wa eneo hilo.

Alikiri na kusema barabara nyingi zinazokwenda katika hoteli hizo ziko katika hali mbaya zikiwa zimejengwa kwa kutiwa kifusi na wakati mwingine kusababisha vumbi.

"Mheshimiwa Spika nafahamu barabara za ndani zinazokwenda katika miradi ya hoteli za kitalii zilizoko Nungwi ziko katika hali mbaya. Tunatafuta fedha kwa ajili ya kuzikarabati," alisema.

Pia waziri huyo ameupongeza uongozi wa hoteli ya Kendwa –Zuru, Nungwi kwa kujenga barabara inayofika eneo hilo yenye urefu wa kilometa 2.7 kwa kiwango cha lami na kuwezesha kufikiwa vizuri.

Hata hivyo, alisema matarajio makubwa ya wizara ni utekelezaji wa mradi mkubwa wa Big-Z ulioko chini ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango wenye lengo la kuimarisha miundombinu ya barabara za vijijini Unguja na Pemba.

**Alikiri na kusema barabara nyingi zinazokwenda katika hoteli hizo ziko katika hali mbaya zikiwa zimejengwa kwa kutiwa kifusi na wakati mwingine kusababisha vumbi.**



Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini Machano Othmad Said akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana huko Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mwinyi atia saini muswada dawa za kulevya

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, amesema miswada miwili iliyopitishwa katika mkutano uliopita mwishoni mwa mwaka jana, imetiwa saini na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na kuwa sheria kamili.

Kutokana na kutiwa saini na Rais, miswada hiyo sasa ni sheria ambazo utekelezaji wake unaanza mara moja.

Akizungumza jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Spika aliitaja miswada hiyo iliyopitishwa Desemba 15, 2021 ukiwamo wa sheria mbalimbali pamoja na muswada wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Alisema hatua hiyo ni kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu cha 92(3) ambayo miswada yote iliyopitishwa na wajumbe inahitaji kutiwa saini na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

"Napenda niwajulishe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla kwamba miswada iliyopitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilshi sasa ni sheria kamili inayoanza kutekelezwa," alisema.

Aliutaja muswada wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya sasa utaiwezesha taasisi hiyo kufanya kazi zake kikamilifu ikiwamo kukamata, kufanya upelelezi na kufikisha watuhumiwa mahakamani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ESTHER ASHERY** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo kozi ya UALIMU chenye namba za usajili **E539/043** kilichotolewa na chuo cha IFUNDA TEACHERS COLLEGE mwaka 1996,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MAG/RB/687227/2022**

116709202

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODWIN E MUNGURE** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo chenye namba za usajili **DEHS/KGM/16/14** kozi ya ENVIRONMENTAL HEALTH SCIENCE kilichotolewa na chuo cha KAGEMU HEALTH SCIENCE mwaka 2016,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **AR/RB/855/2018**

116708502

## KUPOTEA KWA CHETI



**WINCHSILAUS SEVELIN LAULIAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4165-0073** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya KIHUMULO mwaka 2018,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MBT/RB/483/2022**

116708602

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**
**LAND CASE APPEAL NO. 78 OF 2021**
**(Arising from DLHT of Bukoba Appl No. 236 of 2010 and Land case No. 85 of 2010 of Kahororo Ward Tribunal)**

**GOSBERT KAHWA ....................................................1ST APPELLANT**
**SULEIMAN BUGOHWE .........................................2ND APPELLANT**
**JACKEM AUCTION MART & COURT BROCKERS LTD .....3RD APPELLANT**

**VERSUS**

**MSAFIRI M MALANJA ................................................RESPONDENT**

**TO, MSAFIRI M MALANJA**
**OF KAHORORO WARD**
**BUKOBA MUNICIPAL**
**MOBILE 0782432589**

**RE: NOTICE FOR DATE OF HEARING**

Whereas the above mentioned Appellants have lodged an appeal registered as Land Case Appeal No. 78 of 2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for hearing on 9th day of March, 2022 at 08:30 am before Honourable Ngigwana J. You are required to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the hearing, the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 9th day of February, 2022.

HIGH COURT OF TANZANIA BUKOBA

ODIRA AMWORO
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

116710302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU ABEDNEGO CRISPIN MHAGAMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T520DBZ** aina ya **TOYOTA RUNX,** Rangi Silver yenye Chasis No.**NZE-121-5048887,** Engine **No.1NZ-FE1496.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DAR/MAG/RB/502595/2020**

11709402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi......5..2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU MICHAEL BLASS SHAYO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA HUSNA JUMA OMARY.**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 04/03/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe04/02/2022**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116709002

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MATIMBWA MOHAMED MATIMBWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 737 CLM.** ENGINE NO **SR162FMJ 19708034.** CHASSIS NO **ID3PCK6JOK2012198.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. **ARU/KIK/RB/9344/2022.**

116708702

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Algeria kutoa dola 100 kwa mwezi wasio na ajira

**ALGIERS,** ALGERIA

RAIS wa Algeria, Abdelmadjid Tebboune amesema serikali itaanzisha mafao ya ukosefu wa ajira kwa vijana, wakati nchi hiyo ikipambana na viwango vya juu vya ukosefu wa ajira.

Rais aliwaambia waandishi wa habari kwamba malipo kwa watafuta kazi wenye umri wa miaka 19 hadi 40 yataanza mwezi Machi, mwaka huu.

Alisema, wale ambao wamehitimu wataweza kukusanya malipo ya takriban dola 100 kwa mwezi, pamoja na baadhi ya mafao ya matibabu, hadi wapate kazi.

Akitoa tangazo hilo, Rais Tebboune alisema, Algeria ilikuwa nchi ya kwanza nje ya Ulaya kuanzisha mpango huo. Aliongeza kwamba, sasa kuna zaidi ya watu 600,000 hawana ajira. **BBC**

## AMNESTY yatuhumu waasi Tigray ubakaji

**LONDON,** UINGEREZA

RIPOTI ya shirika la kutetea haki za binadamu la Amnesty International, limebaini ukiukwaji mkubwa wa sheria ya haki za kibinadamu, unaofanywa na wapiganaji waasi kutoka eneo la Tigray nchini Ethiopia.

Ripoti hiyo inawashutumu waasi wa Tigray kwa ubakaji wa genge na mauaji ya kimakusudi ya raia katika eneo jirani la Amhara, ambako walidhibiti eneo hilo kwa muda hadi walipoondolewa na vikosi vya serikali, miezi miwili iliyopita.

Amnesty ilisema, vikosi vya waasi viliua raia wasiokuwa na silaha katika mji wa Kobo na kuwanyanyasa kingono takriban wanawake na wasichana 30 katika kijiji cha Chena.

Mali za umma, ikiwa ni pamoja na shule na vituo vya matibabu viliporwa au kuharibiwa.

Hata hivyo, kundi la The Tigray People Liberation Front (TPLF), halijajibu madai ya hivi punde. Limekanusha shutuma kama hizo hapo awali. **BBC**

# ‘Hausigeli’ atolewa figo na mwajiri ughaibuni

**Kampala,** UGANDA

MADAKTARI wamethibitisha kwamba, mwanamke aliyekuwa akifanya kazi za nyumbani nchini Saudi Arabia, ameondolewa figo yake ya kulia na chanzo haikuwa ajali ya gari, kama ilivyoarifiwa awali na mwajiri wake.

Wizara ya Mambo ya Ndani Uganda, imethibitisha hilo, baada ya kupewa ripoti ya uchunguzi kutoka Hospitali kuu ya kitaifa ya Mulago.

Kutokana na taarifa hiyo, familia ya mwanamke huyo inaiomba serikali kusimamia suala hilo hadi haki itakapopatikana.

Judith Nakintu, (38) ana watoto watano na alichukuliwa na kampuni ya Nile Treasure Gate, mwaka 2019 kwa ajili ya kwenda kufanya kazi za nyumbani huko Jeddah, nchini Saudi Arabia.

Baada ya kufanya kazi karibu miezi miwili, mawasiliano yake na familia yake yalikatika, ndipo mama yake mzazi alipoanza kufuatilia karibu miezi mitatu, ndipo akaambiwa mwanae amepata ajali.

**Alitufahamisha kwa simu kwamba alipata ajali nilikuwa nataka kufahamu familia yake, nikamuuliza alipata ajali bila kampuni iliyompeleka kujua?**

“Alitufahamisha kwa simu kwamba alipata ajali nilikuwa nataka kufahamu familia yake, nikamuuliza alipata ajali bila kampuni iliyompeleka kujua? Nikawapigia simu kampuni yake nikawaeleza, wakasema hawana habari wala taarifa,” alisema mama huyo.

Kampuni ya Nile Treasure Gate, ilimpigia mama wa Nakintu simu, Oktoba 30 mwaka jana. Mwanae alikuwa anatarajia kuwasili katika uwanja wa ndege wa Entebe siku hiyo. Aliondoka mpaka kwenye uwanja huo wa ndege kwa ajili ya kumpokea mwanae.

Alipowasili alimuona mwanae akiletwa kutoka kwenye ndege akiwa kwenye kiti cha wagonjwa cha magurudumu, hawezi kutembea na kuingizwa kwenye gari la wagonjwa hadi Hospitali kuu ya Mulago.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na mtandao wa Indepent, Kampuni ya Nile Treasurer, siku chache baadaye ilipokea taarifa kuwa watoto wawili wa waajiri hao wamefariki dunia kutokana na ajali hiyo, bahati nzuri Nakintu alinusurika ingawa ameumia sana na kusababisha damu yake kuganda.

Kwa upande wake, Rais wa Migrant Workers Voice, inayoshughulikia masuala ya Wafanyakazi Wahamiaji, Abdallah Kayonde, alisema ameiandikia kampuni hiyo kulipa fidia ya shilingi milioni 600 za Uganda, kwa kitendo cha kutolewa figo Nakintu, kinyume cha sheria na kuiuza.

Hata hivyo, kampuni hiyo imenukuliwa ikipinga kuhusika na kutolewa kwa figo ya mwanamke huyo. **BBC**



Treni ya mizigo ikiwa imebeba magari na vifaa vya kijeshi vya jeshi la Urusi, Vikosi hivyo vimeondolewa peninsula ya Crimea kando ya daraja kuvuka lango la bahari ya Kerch Strait, kuelekea nchini Urusi, jana. **PICHA: REUTERS**

# Urusi yaondoa wanajeshi mpakani baada ya luteka

**MOSCOW,** URUSI

URUSI, inaendelea kuwaondoa wanajeshi wake karibu na mpaka wa Ukraine, baada ya kukamilika kwa luteka za kijeshi.

Ukraine na nchi za Magharibi, zimesema ni vigumu kuyaamini madai hayo ya Urusi.

Wizara ya Ulinzi Urusi, ilisema vikosi kadhaa vilivyohusika katika mazoezi ya rasi ya Bahari Nyeusi ya Crimea, ambayo Urusi iliichukua kimabavu kutoka Ukraine mwaka wa 2014, sasa vimerejea makambini.

Shirika la habari la serikali, Ria Novosti, lilitoa video ikionyesha msafara wa vifaru na magari mengine ya kijeshi yakisafiri gizani kwenye daraja la Crimea linalounganisha rasi hiyo na Urusi.

Wizara hiyo, haikutoa maelezo zaidi kuhusu aina ya wanajeshi walioondolewa na idadi ya askari waliohusika.

Hatua hiyo, inaleta matumaini madogo ya mzozo huo kwenye mpaka wa Ukraine, baada ya wiki kadhaa za shughuli lukuki za kidiplomasia na vitisho kutoka kwa nchi za Magharibi vya kutangaza vikwazo vikali kama Urusi itaivamia Ukraine.

Wasiwasi kuhusu nia ya Moscow, bado ni mkubwa. Ukraine, Marekani, madola ya Ulaya na Jumuiya ya Kujihami (NATO), wote wamedokeza kuwa hawawezi kuiamini Urusi moja kwa moja, kwa inachosema na kuwa wanahitaji uthibitisho huru.

Rais wa Halmashauri Kuu ya Ulaya, Ursula von der Leyen, alisema Urusi bado inahitaji kuthibitisha kama iko tayari kuutuliza mzozo.

Von der Leyen, aliwaambia wabunge wa Ulaya kwamba, Moscow inatuma ishara zinazokinzana, akimaanisha masharti ya Bunge la Urusi ya kuyatambua majimbo ya Mashariki mwa Ukraine ya Donetsk na Luhansk pamoja na kauli ya mkuu wa NATO, Jens Stoltenberg, iliyosema bado hawajaona ushahidi wa kupungua vikosi vya Urusi mpakani.

Mjini Brussels, mawaziri wa ulinzi wa nchi 30 wanachama wa NATO, akiwamo Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, watajadili mipango ya hatua zaidi za kuizuia Urusi dhidi ya kuivamia Ukraine.

Washirika wa NATO, wamekuwa wakipeleka manowari zaidi, ndege za kivita na askari Mashariki mwa Ulaya na kuwaweka wanajeshi wengine katika hali ya kuwa tayari kutumwa vitani.

Wakati huo huo, Ukraine imeadhimisha siku ya umoja. Rais Volodymyr Zelensky, aliitangaza siku hiyo mapema wiki hii baada ya ripoti katika vyombo vya Habari vya Marekani kutaja Februari 16, kuwa siku ambayo Urusi ingefanya uvamizi.

Waukraine walipeperusha bendera za taifa na kucheza wimbo wa taifa, kuonyesha umoja dhidi ya kitisho cha uvamizi wa Urusi.

Rangi za taifa za njano na bluu, zilishamiri kila mahali kuanzia shuleni, hospitalini hadi nje ya maduka. **DW**

# KILI MARATHON YATANGAZA VITUO VYA KUTOLEA NAMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDAAJI wa mbio za 20 za Kilimanjaro Premium Lager Marathon wametangaza vituo vitatu vya kutolea namba za kukimbilia ambavyo viko Dar es Salaam, Arusha na Moshi.

Taarifa iliyotolewa jana ilisema zoezi hilo litafanyika Jumamosi na Jumapili katika viwanja vya Mlimani City jijini Dar es Salaam kuanzia saa 6:00 mchana hadi saa 12:00 jioni kwa siku zote mbili.

"Tunatoa wito kwa wakazi wa Dar es Salaam ambao wamejisajili wajitokeze kwa wingi kuchukua namba zao pamoja na vesti za kukimbilia kwa siku hizo mbili zilizotengwa," ilisema taarifa ya waandaaji hao.

Iliongeza baada ya Dar es Salaam, zoezi hilo litahamia Arusha katika hoteli ya Kibo Palace Jumanne na Jumatano ijayo kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa moja usiku.

Taarifa hiyo ilisema zoezi hilo litamalizika katika mji wa Moshi ambapo namba hizo zitatolewa katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Februari 24, 2022 kuanzia saa 6:00 mchana hadi Februari 25, mwaka huu, saa 12:00 jioni huku Februari 26, likifanyika kati ya saa 3:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

"Washiriki waliojisajili wanatakiwa kuzingatia muda wa zoezi hili katika vituo husika ili kuepusha usumbufu na zoezi likishafungwa hakutakuwa na ugawaji wa namba siku ya mashindano," walisema waandaaji hao.

Waliongeza usajili kwa ajili ya mbio za kilomita 5 bado unaendelea kwa njia ya Tigo Pesa kwa kubonyeza *149*20# na usajili huo pia utafanyika katika vituo vya kutolea namba.

"Tumefunga usajili kwa ajili ya kilomita 42 na kilomita 21 kwa sababu nafasi zimejaa lakini ule wa kilomita tano bado unaendelea," waliongeza waratibu.

> **Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Irene Mutiganzi, ambao ni wadhamini wakuu wa mbio hizi, alitoa wito kwa washiriki wajitokeze kwa wingi kuchukua namba zao tayari kwa mashindano ya wiki ijayo.**

"Waandaaji wametenga muda wa kutosha wa zoezi hili la kugawa namba kwa Dar es Salaam, Arusha na Moshi kama wadhamini wakuu tunatoa rai kwa washiriki wajitokeze mapema ili kuepusha usumbufu dakika za mwisho," alisema na kuongeza wamejiandaa vizuri kuadhimisha miaka 20 ya Kilimanjaro Marathon.

Wadhamini wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 ni Kilimanjaro Premium Lager (Mdhamini Mkuu), Kampuni ya Tigo wanaodhamini mbio za kilomita 21 na Grand Malt wao wanadhamini mbio za kilomita tano.

Wadhamini wa meza za maji ni pamoja na Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement na Maji ya Kilimanjaro huku wasambazaji rasmi ni Garda-World Security, hoteli ya Keys, Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles na Surveyed Plots Company Ltd (SPC) na Bodi ya Utalii (TTB).

Katika hatua nyingine, Kwa mujibu wa waandaaji wa Kilimanjaro Marathon, kwa mara ya kwanza kutakuwepo na maonyesho yanayojulikana kama Kili Expo (The People's Expo) ambapo wadhamini na wadau wengine wa mbio hizo watapata fursa ya siku tatu za kuonyesha bidhaa na huduma wanazotoa, maonyesho ambayo yanatarajiwa kufanyika kati ya Februari 24 na 26, 2022 kwenye viwanja vya MoCU.

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zitafanyika Februari 27, mwaka huu, katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), ambapo zimeandaliwa na Taasisi ya Kilimanjaro Company Limited na kuratibiwa na wadau wa hapa nchini kampuni ya Executive Solutions Limited.



Wachezaji wa Yanga wakiwa wamevaa jezi maalumu kabla ya mechi dhidi ya Biashara United zilizoandikwa jina la mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Ally Mtoni 'Sonso' ili kumwenzi beki huyo aliyefariki wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

# Azam FC, Pamba kunoa makali leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Azam FC kinatarajia kwenda kuweka kambi ya siku nne jijini Mwanza na kikiwa huko kimepanga kucheza mechi moja ya kirafiki dhidi ya Pamba inayoshiriki Ligi ya Championship zamani Ligi Daraja la Kwanza imeelezwa.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabiti Zakaria 'Zaka', alisema timu yao iliondoka jijini Dar es Salaam jana na ikiwa Mwanza lengo la mchezo huo wa kirafiki ni kujiandaa na mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United itakayochezwa Februari 22, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Karume ulioko Musoma, Mara.

Zaka alisema mechi hiyo ya kirafiki dhidi ya Pamba FC itachezwa leo na inatarajia Februari 20, mwaka huu, itaondoka kuelekea Musoma kwa ajili ya kufuata pointi tatu kutoka kwa wenyeji Biashara United.

Kuhusu suala la Uwanja wa Karume ambao watautumia kwa ajili ya mchezo huo kutokuwa rafiki, alisema wanazitaka mamkala husika kuliangalia kwa umakini uamuzi wa kuendelea kuutumia uwanja huo.

"Azam FC tuliwatuma maofisa wetu kwenda kukagua uwanja na kuonekana sio rafiki kuchezea, haujafanyiwa ukarabati, mamlaka husika wafanyie kazi hilo haraka la kupata kiwanja ambacho kitakuwa na hadhi ya kuchezea ligi," alisema Zaka.

## Kiduku, Kabangu kuzipiga Machi 26

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Twaha Kiduku, anatarajia kupambana na Mkongomani Alex Kabangu katika pambano litakalofanyika Machi 26, mwaka huu mkoani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kiduku alisema ana imani atafanya vizuri katika pambano hilo kutokana na maandalizi mazuri anayofanya kuelekea mtanange huo.

Kiduku alisema sapoti anayopewa na Watanzania inazidi kumpa nguvu ya kujipanga kuendeleza historia ya kumchakaza Kabangu mara nyingi.

"Ni kweli nimesaini kucheza pambano hilo, litakuwa la mkanda wa ubingwa, naamini mkanda utabaki nyumbani kwa sababu lazima nifanye maandalizi ya kutosha chini ya kocha wangi Pawa Ilanda," alisema Kiduku.

Alisema siku hiyo kutakuwa na mapambano mengine ya utangulizi ambapo bondia Joseph Mchapeni atapambana na Ally Mwerangi huku Juma Misari atazichapa na Kareem Mandonga, wote wanatoka Morogoro.

## Ubovu Sokoine waibeba Polisi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema ubovu wa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya ulisababisha wabadili mfumo wa uchezaji ambao uliwapa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya wenyeji Prisons, ikiwa ni mechi ya hatua ya 16 bora ya mashindano ya Kombe la FA.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa juzi, Malale alisema siku moja kabla ya mechi walikwenda kwenye Uwanja wa Sokoine kuangalia hali ilivyo, lakini hakuridhishwa nayo kutokana na hali ya mvua kunyesha jijini humo.

"Baada ya kuona uwanja haufai, nikaamua kucheza mipira mirefu na kujaza washambuliaji mbele bila viungo wengi, na watu wa mbele walikuwa warefu, kwa hiyo kazi yao ilikuwa ni kupokea mipira kutoka nyuma na kuituliza, kusubiri wengine wasogee na kuwapasia," alisema Malale.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Prisons, Patrick Odhiambo, alisema makosa ya mabeki wake kutowasiliana vizuri na kipa, ndiyo yaliyoigharimu timu hiyo.

"Goli la kwanza tulilofungwa kwa haraka sana ndilo lililowatoa wachezaji wangu kwenye mchezo. Tumefungwa goli la mapema sana, na ilikuwa ni kutowasiliana kati ya mabeki wangu na kipa, baada ya hapo hakutuwa kwenye mchezo, tukafungwa la pili," alisema kocha huyo wa zamani wa Biashara United.

## ZISIKUPITE

### RONALDO AGOMBEWA ULAYA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, anazivutia pumzi klabu za Paris St-Germain, Bayern Munich na AS Roma wakati huu akitafakari kuhusu kuondoka Old Trafford msimu huu. (***Sun***)

### SAVIO ATAKIWA CITY

MANCHESTER City imetenga ofa ya pauni milioni 5.5 kwa ajili ya winga wa Atletico Mineiro, Savio. Kinda huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 17, anasakwa pia na Arsenal. (***Guardian***)

### VILLA YASAKA KIUNGO

KLABU ya Aston Villa iko tayari kutumia pauni milioni 50 kununua kiungo huku viungo walioko kwenye orodha ya juu kusakwa ni kiungo wa kimataifa wa Nigeria na Leicester, Wilfred Ndidi mwenye umri wa miaka 25 na kiungo wa Brighton na Mali, Yves Bissouma (25). (***Star***)

### BOWEN ANUKIA WEST

WEST Ham inapanga kuzungumza na kiungo, Jarrod Bowen mwenye umri wa miaka 25 mwishoni mwa msimu huu, kuhusu mkataba mpya ili kuzuia kusajiliwa na Liverpool wanaomsaka. (***Evening Standard***)

### BROJA AWEKWA SOKONI

BAYERN Munich na Borussia Dortmund ni klabu za hivi karibuni zinazomfuatilia mshambuliaji wa Chelsea na Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, ambaye anacheza kwa mkopo Southampton. (***Sun***)

### LIVERPOOL, CHELSEA VITANI

MANCHESTER United, Liverpool, Chelsea, Arsenal na Newcastle zinafuatilia kinachoendelea kuhusu mkataba wa Kalvin Phillips pale Leeds. Mkataba wa kiungo huyo wa England mwenye umri wa miaka 26 unamalizika mwaka 2024. (***90min***)

### CHELSEA YAMTAKA KOUNDE

CHELSEA inataka kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23 kutoka Sevilla baada ya kutaarifiwa kuwa Paris St-Germain haitamuuza beki wake wa kati, Marquinhos mwenye umri wa miaka 27. (***Fabrizio Romano***)

### TIELEMANS KUTUA CHELSEA

KIUNGO wa Leicester City, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ubelgiji ametakiwa kukacha kuhamia klabu za Liverpool na Manchester United ili kujiunga na Chelsea, kwa mujibu wa kiungo wa zamani wa United na Brazil, Kleberson. (***Express***)

### MILNER MAMBO SAFI

LIVERPOOL ipo kwenye mazungumzo na kiungo wa zamani wa England, James Milner mwenye umri wa miaka 36, kuhusu kumwongezea mkataba wa mwaka mmoja. (***Fabrizio Romano***)

### MASSENGO AINGIA SOKONI

Leicester City na Southampton zinamwania kiungo Mfaransa wa Bristol City, Han-Noah Massengo mwenye umri wa miaka 20. (***Football Insider***)

### RICE ATAJWA CHELSEA

MLINZI wa zamani wa West Ham na Chelsea, Glen Johnson amesema timu yake hiyo inapaswa kumsajili nyota wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23 kutoka West Ham kuziba nafasi ya kiungo wa kimataifa wa Italia, Jorginho (30). (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AFUNGUKA KUHUSU UBORA WAKE

**Mfaransa huyo asema amethibitisha kiwango chake katika mchezo dhidi...**

**PARIS,** UFARANSA

KYLIAN Mbappe anaamini kiwango chake alichokionyesha na bao la ushindi alilofunga dhidi ya Real Madrid limethibitisha majukumu yake ndani ya Paris Saint-Germain - ingawa alikataa kuzima uvumi kuhusu majaliwa yake ya baadaye.

Wakati wa maandalizi ya mchezo huo wa hatua ya 16 wa Ligi ya mabingwa Ulaya kati ya PSG na Madrid habari kubwa ilikuwa ni kuhusu Mbappe ambaye anawaniwa na Los Blancos hao kwa muda mrefu.

Nyota huyo wa Ufaransa yupo kwenye miezi yake ya mwisho kwenye mkataba wake na PSG, na kwa mujibu wa ripoti kuna uwezekano mkubwa akajiunga na Madrid mwishoni mwa msimu huu.

Lakini mara zote amekuwa akizungumzia kuhusu majukumu yake ndani ya PSG na kwamba kwa sababu anavaa jezi ya timu hiyo atajitoa kwa hali na mali na juzi Jumanne alionyesha kiwango cha kuvutia wakati wakiibuka na ushindi huo wa bao 1-0.

**Mbappe alipiga mashut i saba kwenye mchezo huo, ambapo mengine yal iokolewa na golikipa , Thibaut Courtois na pia alipata pen alti ambayo Lionel Messi aliikosa.**

Na wakati Madrid walionekana wataondoka na pointi moja kwenye mchezo huo, Mbappe aliwazidi akili mabeki na kupiga shuti lililompita katikati ya miguu Courtois na kufunga bao pekee kwenye mchezo huo, na kuipa nafasi nzuri PSG kwenye mchezo wa marudiano utakaopigwa Machi 9, mwaka huu.

Alipoulizwa amewezaje kupuuzia uvumi unaozagaa kuhusu majaliwa yake kuelekea mchezo huo, Mbappe aliiambia Canal Plus: "Ni rahisi, unatakiwa kucheza soka.

"Tunauliza maswali mengi, tunasema vitu vingi. Tunazungumza kuhusu PSG na Madrid, klabu mbili kubwa. Mimi ni mchezaji wa PSG, mara zote mimi nina furaha sana.

"Nilisema nitakwenda kuthibitisha majukumu yangu na nimethibitisha vizuri kabisa. Nimefanya hivyo kwa mara ya kwanza, tutatakiwa kuthibitisha kwa mara ya pili kule Santiago Bernabeu.

"Tulitaka kuwa tayari kwa vitu vikubwa usiku ule. Tuliota ndoto kuhusu usiku kama huu. Tulitaka kushinda, tulisukumwa na mashabiki wetu."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 940

MECHI KALI
BARCELONA
VERSUS
NAPOLI
1 | 2.02
X | 3.47
2 | 3.62

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# MOURINHO AWANIA KUMSAJILI RONALDO

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo alimaliza ukame wa kutofunga mechi sita Jumanne baada ya kufunga kwenye ushindi dhidi ya Brighton and Hove Albion katika mchezo wa Ligi Kuu England, lakini fowadi huyo wa Manchester United majaliwa yake bado hayajajulikana.


Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or yupo kwa mara ya pili na kikosi hicho cha pale Old Trafford baada ya kukichezea kwa mafanikio makubwa wakati alipotua hapo kwa mara ya kwanza.

Kama ripoti zinazosambaa zitakuwa na ukweli, basi kuna uwezekano mkubwa nyota huyo akaungana na kocha wake wa zamani, Jose Mourinho kule Italia ndani ya miezi ijayo.

Roma ni moja kati ya klabu tatu zinawania huduma ya Ronaldo kama ataondoka Manchester United kwa mujibu wa The Sun.

Mourinho ambaye ni kocha wa AS Roma awali alimnoa Ronaldo akiwa Real Madrid na sasa anawaniwa kumsajili tena.

Hata hivyo, haijulikani kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 atakubali kurudi tena kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.




# Bao la Silva lamkuna Pep Guardiola

**LISBON,** Ureno

PEP Guardiola alizingatia bao la kwanza la Bernardo Silva dhidi ya Sporting CP Jumanne kuwa "moja ya bao bora zaidi kuwahi kuliona".

Silva, mchezaji wa zamani wa Benfica alirejea Lisbon, alifunga mabao mawili katika ushindi wa mabao 5-0 wa Manchester City dhidi ya Sporting katika mchezo wa kwanza hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ubora wa mchezo huo ulianza dakika ya 17 ambapo kiungo huyo wa City alipiga shuti kali nje ya 18 na kufunga bao lililowafanya wageni kuwa mbel

Silva alikuwa hajafunga b
la Ligi ya Mabingwa Ulaya ta
gu hatua hiyo ya michuano
mwaka jana, huku mabao ya
mawili Jumanne yakimaa
sha kuwa ana matano kati
nane aliyoifunga City kwen
kinyang'anyiro hicho.

Hili lilikuwa bao la kwan
kabisa kwa Silva katika Ligi
Mabingwa Ulaya na lilimfan
afikishe mabao 10 kwa msi
huu katika mashindano yo
idadi yake kubwa zaidi kati
msimu mmoja tangu alipofan
hivyo msimu wa 2018-19 alip
funga mabao 13.

,850,660

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/02/22 | 18:00 | Zaragoza vs Las Palmas UD | 2.80 | 3.19 | 2.44 |
| 02. 19/02/22 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich | 2.74 | 3.03 | 2.59 |
| 03. 19/02/22 | 19:00 | Lens vs Lyon | 2.75 | 3.40 | 2.46 |
| 04. 19/02/22 | 20:30 | Oostende vs Standard Liege | 2.55 | 3.34 | 2.60 |
| 05. 19/02/22 | 20:30 | Cadiz CF vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.55 |
| 06. 19/02/22 | 21:00 | Niort vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.95 | 2.70 |
| 07. 20/02/22 | 13:30 | Gaziantep BB vs Adana Demirspor | 2.58 | 3.27 | 2.63 |
| 08. 20/02/22 | 14:15 | PEC Zwolle vs Groningen | 2.38 | 3.24 | 2.85 |
| 09. 20/02/22 | 14:30 | Fiorentina vs Atalanta | 2.85 | 3.45 | 2.38 |
| 10. 20/02/22 | 16:00 | Fatih Karagumruk vs Sivasspor | 2.60 | 3.19 | 2.65 |
| 11. 20/02/22 | 17:00 | Venezia vs Genoa | 2.55 | 3.21 | 2.80 |
| 12. 20/02/22 | 18:30 | Maritimo vs Famalicao | 2.39 | 3.26 | 2.86 |
| 13. 20/02/22 | 19:30 | Wolverhampton vs Leicester | 2.42 | 3.15 | 3.05 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 17/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3304 | Bandirmaspor vs Manisa BBSK | 2.23 | 3.33 | 2.85 |
| 14:30 | 3919 | Hellas Verona Youth vs Spal Youth | 2.01 | 3.47 | 3.18 |
| 14:30 | 4371 | Umraniyespor vs Adanaspor | 1.36 | 4.44 | 7.14 |
| 14:30 | 5565 | Rahmatgonj Mfs vs Sheikh Jamal | 6.38 | 4.45 | 1.39 |
| 15:00 | 1987 | Jezero vs Decic Tuzi | 4.73 | 3.57 | 1.64 |
| 15:30 | 4672 | Tuna Luso PA vs Castanhal EC PA | 1.85 | 3.26 | 3.94 |
| 15:45 | 2127 | AL Baten vs Al Nasr Riyadh | 4.84 | 4.05 | 1.62 |
| 16:00 | 1251 | Etincelles vs Bugesera FC | 2.83 | 2.88 | 2.50 |
| 16:00 | 2843 | Espoir FC vs Police FC Rwanda | 3.85 | 3.00 | 2.13 |
| 16:00 | 5554 | Saint George FC vs Hadiya Hosahina FC | 1.51 | 3.70 | 5.96 |
| 16:00 | 5803 | Rayon Sports FC vs Rutsiro FC | 1.82 | 3.23 | 4.14 |
| 16:30 | 2365 | Bologna Youth vs US Lecce youth | 2.64 | 3.61 | 2.25 |
| 17:00 | 1999 | Jamshedpur vs Mumbai City FC | 2.74 | 3.31 | 2.31 |
| 17:00 | 3204 | Erzurum BB vs Eyupspor | 1.97 | 3.42 | 3.32 |
| 17:00 | 3546 | Shabab AL Amari vs Hilal Al-Quds | 4.99 | 4.03 | 1.54 |
| 17:00 | 5519 | Shabab Al Dhahiriya vs Markez Balata | 2.85 | 3.14 | 2.33 |
| 18:00 | 1465 | Domzale vs Olimpija Ljubljana | 3.23 | 3.18 | 2.10 |
| 18:00 | 2554 | Akwa Starlets FC vs Gombe United FC | 1.69 | 3.23 | 5.02 |
| 18:00 | 4573 | Al Sadd SC vs Qatar SC | 1.12 | 7.74 | 12.57 |
| 18:05 | 4722 | Kazma SC vs Yarmouk | 1.22 | 5.79 | 9.47 |
| 18:30 | 1434 | Al Masry Club vs Ceramica Cleopatra | 2.16 | 2.90 | 3.74 |
| 18:30 | 4541 | Varzim vs Sporting Farense | 3.05 | 3.20 | 2.39 |
| 18:35 | 4326 | Al Taawon vs Al Ittihad Jeddah | 5.54 | 4.36 | 1.51 |
| 18:55 | 5838 | Al Ahli Jeddah vs AL Faiha | 2.03 | 3.68 | 3.28 |
| 19:00 | 4214 | Heartland FC Owerri vs Lobi Stars | 2.01 | 3.15 | 4.10 |
| 19:00 | 5706 | Apoel Nicosia vs Anorthosis Famagusta | 1.98 | 3.32 | 3.77 |
| 19:00 | 5749 | Adama City FC vs Mekelakeya | 2.16 | 2.94 | 3.37 |
| 20:00 | 1321 | Juventus U23 vs Piacenza Calcio | 2.27 | 3.08 | 3.28 |
| 20:40 | 5560 | Al Hilal Riyadh vs Al Shabab Riyadh | 2.03 | 3.62 | 3.32 |
| 20:45 | 1126 | Midtjylland vs PAOK | 2.08 | 3.40 | 3.50 |
| 20:45 | 1413 | PSV Eindhoven vs Maccabi Tel Aviv | 1.29 | 5.60 | 9.40 |
| 20:45 | 2699 | Fenerbahce vs Slavia Prague | 2.10 | 3.40 | 3.45 |
| 20:45 | 2723 | Borussia Dortmund vs Rangers | 1.39 | 4.99 | 7.19 |
| 20:45 | 3576 | Zenit St Petersburg vs Betis | 2.49 | 3.40 | 2.75 |
| 20:45 | 4890 | Sheriff Tiraspol vs Sporting Braga | 3.64 | 3.39 | 2.04 |
| 20:45 | 5045 | Barcelona vs Napoli | 2.02 | 3.47 | 3.62 |
| 20:45 | 5652 | Rapid Vienna vs Vitesse Arnhem | 2.33 | 3.44 | 2.94 |
| 21:00 | 5965 | Clinceni vs Farul Constanta | 23.54 | 7.85 | 1.10 |
| 22:00 | 2892 | Patriotas FC vs Once Caldas | 2.90 | 3.20 | 2.50 |
| 22:00 | 5269 | Portuguesa RJ vs Boavista RJ | 2.00 | 3.08 | 3.61 |
| 23:00 | 1018 | Pescara Calcio vs Virtus Entella | 2.43 | 3.31 | 2.81 |
| 23:00 | 1166 | Marseille vs Karabakh | 1.35 | 5.01 | 8.22 |
| 23:00 | 1785 | Atalanta vs Olympiakos | 1.48 | 4.52 | 6.22 |
| 23:00 | 2109 | Sevilla FC vs Dinamo Zagreb | 1.37 | 4.81 | 8.02 |
| 23:00 | 3247 | Sparta Prague vs Partizan | 2.04 | 3.49 | 3.54 |
| 23:00 | 3260 | Celtic vs Bodo Glimt | 1.45 | 4.59 | 6.59 |
| 23:00 | 3472 | Leicester vs Randers | 1.27 | 5.78 | 9.76 |
| 23:00 | 4270 | Porto vs Lazio | 2.13 | 3.46 | 3.31 |
| 23:00 | 5436 | Colon Santa Fe vs Godoy Cruz | 2.02 | 3.19 | 3.43 |
| 23:00 | 5872 | RB Leipzig vs Real Sociedad | 1.91 | 3.59 | 3.89 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MAJERUHI SIMBA, YANGA KILIO KINACHOWAANDAMA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuendelea kufanya vyema katika michuano mbalimbali, klabu kongwe za Simba na Yanga zinakabiliwa na changamoto ya idadi kubwa ya majeruhi ambao wanasababisha wakati mwingine wasiwe kwenye ubora wao wa kawaida.

**Wakati Yanga ikitangaza kuwa na majeruhi 12, Simba yenyewe imetangaza nyota wake, Chris Mugalu na Hassan Dilunga wameongeza idadi ya majeruhi kwenye kikosi chao.**

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema kuumia kwa Jesus Moloko katika mechi ya raundi ya tano ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, kumesababisha idadi ya majeruhi walionao kufikia 12.

"Tuna changamoto ya majeruhi wengi, unaona kikosi kimebadilika sana leo (juzi), Farid Mussa amecheza beki wa kushoto kwa sababu hakukuwa na mchezaji mwingine anayeweza kucheza, tena Moloko ameumia, kwa hivyo ameongeza idadi ya majeruhi tulionao, hii inatupa changamoto sana. Lakini nadhani mpaka wiki ijayo, baadhi watakuwa wameanza kurejea," alisema Bumbuli.

Hata hivyo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, hajasema nyota hao watakaa nje kwa muda gani, lakini taarifa za ndani zinasema Mugalu huenda akawa nje kwa wiki mbili huku Dilunga akiwa kwenye chumba cha daktari kiasi cha wiki tatu.

"Mugalu aliumia kidole kwenye mechi dhidi ya Mbeya Kwanza, aligongana na kipa wa timu hiyo, Dilunga yeye aliumia mazoezini wakati tukijiandaa na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas," alisema Ahmed.

Wachezaji hao wanaunga na Denis Kibu ambaye aliumia katika mechi dhidi ya Mbeya City huku Tadeo Lwanga akiwa bado hajaanza kuitumikia timu hiyo kutoka kwenye majeraha.

Baadhi ya majeruhi wa Yanga ni Yacouba Songne, Abdallah Shaibu 'Ninja' na Kibwana Shomari.



Waamuzi wanaochezesha mechi za Ligi Kuu na Championship wakiwa na wakufunzi wao baada ya kumaliza semina ya siku tatu iliyofanyika kwenye ukumbi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# *Zanzibar yawakumbuka yosso*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Soka la Vijana ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imefanya ziara maalumu kwa klabu 12 zinazoshiriki Ligi Kuu visiwani hapa ili kufahamu programu zake za maendeleo ya timu zao zilizo na wachezaji wa umri chini ya miaka 20.

Katibu wa Kamati ya Soka la Vijana wa ZFF, Abdallah Thabiti, aliliambia gazeti hili jana kamati hiyo imefanya ziara kwa timu zote zilizoko Unguja na zote hilo pia litafanyika na kwa upande wa Pemba.

Thabiti alisema lengo la ziara hiyo ni kufahamu namna wanavyoziendeleza timu hizo na pia kuwapa hamasa kuelekea kwenye maandalizi ya ligi za vijana zinazotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Alisema kamati hiyo kwa kushirikiana na Kamati ya Mashindano, imeona ipo haja ya kuwahamasisha viongozi wa timu hizo kufahamu umuhimu wa kuzilea vyema timu hizo ambazo hutoa wachezaji kujiunga na timu za wakubwa.

Aliongeza kwa sasa wanaandaa mkakati wa kupita katika kila wilaya kukutana na viongozi wa timu za vijana za ngazi ya wilaya, ili kupanga programu za kuendeleza soka hilo linalotegemewa kuibua vipaji.

Pia kiongozi huyo amewaomba wadau wa soka la vijana kutoa ushirikiano kwa ZFF kupitia Kamati ya Soka la Vijana katika kufanya maboresho yatakayosaidia kufikia malengo.

# Michezo

Alhamisi Februari 17, 2022

Nipashe




Mourinho awania kumsajili Ronaldo

UKURASA 22

TUPISHE TUPITE!...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Biashara United, Abdulmajid Mangalo, katika mechi ya michuano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga: Ushindi jadi yetu*

**Na Saada Akida**

## Kocha Nabi pia ajivunia uimara na ubora wa kikosi chake licha...

BAADA ya timu yake kusonga mbele kwenye mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amewapongeza wachezaji wake kujituma na kuonyesha kiwango kizuri katika kila mechi, jambo linalomfanya ajivunie kikosi chake.

**Yanga ilipata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa Kombe la FA hatua ya 16 Bora dhidi ya Biashara United uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku.**

Katika mchezo huo Yannick Bangala na Fiston Mayele walifunga mabao kwa upande wa Yanga huku lile la Biashara United yenye makazi yake Musoma likipachikwa wavuni na Collins Opare.

Akizungumza na gazeti hili, Nabi alisema walifanikiwa kupata bao la kwanza na Biashara United wakasawazisha hali ambayo iliwafanya waanze kucheza kwa presha kubwa ili kutafuta ushindi katika michuano hiyo inayochezwa kwa mfumo wa mtoano.

"Hivi karibuni Yanga imekuwa inafungwa na wapinzani wakitangulia mbele au kusawazisha, hayo ni makosa ya mpira huwezi kumlaumu mchezaji yoyote. Najivunia na naweza kusema Yanga ni timu ya ushindi imecheza na kupata matokeo ya ushindi dhidi ya timu imara kama ilivyo Biashara United," alisema Nabi.

Alisema Biashara United imekuwa na mabadiliko makubwa na iliwapa ushindani tofauti na alivyoiona katika mechi zake tatu nyuma za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tumeona mechi ya leo (juzi), wapinzani wetu wamekuwa bora, wachezaji wangu wamepambana na kupata ushindi licha ya kutocheza kwa ubora wao uliozoeleka katika michezo iliyopita," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema pia kukosekana kwa wachezaji wake 10 ambao ni majeruhi kumesababisha kikosi chake kubadilika lakini walipambana na kuonyesha ubora wao.

"Mchezo huu tumekosa wachezaji 10 ambao ni majeruhi lakini na leo (juzi), ameongezeka Jesus Moloko ambaye ameumia na haijajulikana hali yake hadi hapo atakapochunguzwa na daktari na kupata taarifa zake kuhusu mechi ijayo," alisema Nabi.

Kuelekea mchezo ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar alisema wasiwasi pekee waliyonayo ni kuhusiana na hali ya uwanja na tayari leo wanarejea uwanjani kuanza maandalizi ya mechi hiyo inayofuata.

"Tunajua tunatakiwa kuwafuata Mtibwa Sugar, tutajiandaa kuelekea mchezo huo kulingana na mazingira yaliyoko, tunajua kuna changamoto ya uwanja na tutakuwa tayari kukabiliana nayo," Nabi aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati, alisema wachezaji wake walipambana kusaka ushindi lakini Yanga ilitumia makosa yao na kupata mabao yaliyowapeleka hatua nyingine kwenye michuano hiyo.

"Mechi ilikuwa na ushindani na kila timu imecheza vizuri ukizingatia tulifanikiwa kutengeneza nafasi na kupata bao la kusawazisha, lakini Yanga wakatumia mapungufu ya wachezaji wangu kupata bao la pili na kushinda mchezo huu," alisema Vivier.

Yanga yenye pointi 36 ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanajiandaa kuwafuata Mtibwa Sugar kwa ajili ya mechi ya ligi hiyo itakayochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Simba yenye pointi 31 ambao pia ndio mabingwa watetezi wakati Tanzania Prisons wanaburuza mkia wakiwa na pointi 11.

## Simba safarini, Dauda afungiwa

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba wanaondoka nchini kesho na kuelekea Niger kuwafuata US Gendarmarie kwa ajili ya mechi ya pili ya Kundi D ya michuano hiyo itakayochezwa Februari 20, mwaka huu nchini humo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema jana maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na wanafurahi kupata taarifa ya afya ya Pape Ousmane Sakho ambaye aliumia katika mechi iliyopita dhidi ya Asec Mimomas imeimarika.

Ally alisema vipimo vya daktari vimeonyesha Sakho hakupata majeraha makubwa na jana alikuwa na nafasi ya kucheza kama benchi la ufundi linaloongozwa na Mhispania Pabl Franco lingeamua hivyo.

"Baada ya kumaliza mechi yetu dhidi ya Ruvu Shooting, tutajiandaa na safari ya kuelekea Niger. Maandalizi yamekamilika na tunafurahi kuona vipimo vya uchunguzi alivyofanyiwa Sakho ambaye alitoka anachechemea katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi vimetupa majibu mazuri," alisema Ally.

Aliongeza kikosi cha Simba kinaondoka nchini kikiwa na matarajio ya kwenda kufanya vizuri katika mechi hiyo ya pili na kuendelea kujiweka kwenye mazingira bora ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mechi nyingine ya Kundi D itakayochezwa Jumapili itakuwa ni kati ya wenyeji Asec Mimomas ya Ivory Coast dhidi ya RS Berkane kutoka Morocco.

**Wakati huo huo**, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Shaffih Dauda, amefungiwa kujihusisha na mchezo huo kwa muda wa miaka mitano na kutozwa faini ya Sh. milioni sita.

Dauda ambaye pia ni mtangazaji wa kituo cha redio cha Clouds, amekutwa na hatia na Kamati ya Maadili ya TFF katika mashauri mawili yaliyofikishwa kwenye kamati hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >